

TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA (MWALIMU)



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Tatu

TUNAJIFUNZA KUHUSU KANISA VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA (MWALIMU)

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Tatu

**Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study**

J3 - 3Ts

Used by permission of International Publications Services

**Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI**

© Copyright, 1987
Baptist Publications House
All rights reserved

YALIYOMO

SURA

UKURASA

1. Je! Kanisa ni Nini?	5
2. Je! Kanisa Limekuaje?	9
3. Ujumbe Mkuu wa Kanisa	13
4. Je! Naweza Kuwa Mshiriki wa Kanisa?	18
5. Je! Ubatizo Unamaanisha Nini?	22
6. Chakula cha Bwana	26
7. Viongozi wa Kanisa	32
8. Mshuhudie Kristo — Nyumbani	36
9. Mshuhudie Kristo — Kwa Majirani	40
10. Mshuhudie Kristo — Ulimwenguni	46
11. Uwakili wa Maisha	51
12. Mwabudu Mungu	55
13. Kuheshimu Nyumba ya Mungu	60

PALESTINA

Wakati wa Yesu

SCALE OF MILES
0 5 10 15 20 25

Bahari ya Kati

GALLILAYA

Kapernaumu
BAHARI YA GALILAYA

• Nazareti

• Yezreeli

• Bethsaida

• Kaisaria

SAMARIA

• Sukari

Mto Yordani

PEREA

• Yeriko

Yerusalemu



• Mto Olivi

Bethelehemu •

Mto wa Kidroni

• Hebroni

UYAHUDI

• Beersheba

BAHARI YA CHUMVI

SURA YA KWANZA JE! KANISA NI NINI?

MASOMO YA BIBLIA: 1

Wakorintho 12:12-13; 20-27; Mathayo
16:15-18

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! ni yapi wajuayo kuhusu kanisa? Je! Wanalifikiria kanisa kuwa ni jengo tu?

Unapofundisha somo hili utapata nafasi ya kuwaonyesha wanafunzi hao kuwa kanisa si jengo tu. Kanisa ni kundi la waamini ambao wame-mwamini Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi, nao wanamwabudu na kumhudumia. Somo hili litawasaidia wanafunzi kuelewa kwamba Mungu anawaita watu wa kila umri ili wamhudumie. Anawaita vijana, wazee na hata watoto. Kila mtu ni muhimu machoni pa Mungu. Wasaidie wanafunzi wako kuelewa kwamba wanaweza kumhudumia Mungu kanisani. Mwombe Mungu akusaidie kuwaonyesha jinsi wawezavyo kufanya hivyo.

Utapaswa kukazia kwamba tunapaswa kupenda kanisa kwa sababu Kristo alilipenda kwanza. Kristo alilipenda sana kanisa hata akafa kwa ajili yake. Kifungu cha kukumbuka cha somo hili kina-tuambia kwamba Kristo alilipenda kanisa na jinsi sisi tunavyopaswa kulipenda pia.

Unapaswa kusoma na kuelewa maana ya maandiko ili uwaongoze

wanafunzi wako waweze kuelewa maana na kusudi la kanisa.

Soma sura yote ya 1 Wakorintho 12. Wakorintho wa kwanza 12:12-13 inalifanisha kanisa na mwili--mwili wa Kristo. Mwili wa mwanadamu unao viungo vingi, lakini wote ni mwili mmoja tu. Vivyo hivyo, kanisa ni mwili mmoja, lililo na washiriki wengi wenye umri mbalimbali na maisha tofauti. Kila mshiriki wa kanisa ni wa muhimu iwapo yungali kijana au ni mzee, mume au mke. Kifungu cha 13 kinaeleza kwamba rangi au hali ya mtu haimfanyi kuwa tofauti katika ushirika wa kanisa. Watu wa mataifa yote na wa kila aina ni sehemu ya mwili huo mmoja kwa sababu ya imani. Kila mshiriki hupokea karama ya Roho Mtakatifu. Paulo anakazia umoja wa kanisa.

Wakorintho wa Kwanza 12:20-27 inatuambia kwamba sote tunategemeana kama mwili mmoja wa Kristo. Mshiriki mmoja hawezi kumwambia mwenzake kwamba, "Mimi siku-hitaji." Ni lazima washiriki wafanye kazi pamoja kama timu iwapo ni kijana au mzee, mume au mke. Washiriki wenye nguvu wanapaswa kuwa waangalifu kwa washiriki waliodhaifu.

Mungu amempa kila mshiriki wa mwili karama fulani. Karama hizi zinapaswa kutumiwa kwa utukufu wa Mungu na kwa kulijenga kanisa.

Mathayo 16:15-18 inadhihirisha wazi kwamba kanisa lilianzishwa na Kristo. Kanisa si kama chama au ushirika fulani. Mtu anapaswa kuwa na imani kama ya Petro ili awe sehemu ya kanisa. Imani hii ni ile ya kumwamini Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu aishiye. Wakati Yesu alipozungumza juu ya kujenga kanisa lake, hakuwa akizungumza kuhusu jengo la mawe au mbao. Kanisa lake lingekuwa wale wanaompokea kama Mwana wa Mungu na wanatamani kumwabudu na kumtumikia.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi kuelewa maana ya kweli ya kanisa na kujitoa ili wamtumikie Mungu kupitia kwa kanisa.

KULIFUNDISHA SOMO

Waambie wanafunzi wawili wasome sehemu ya mazungumzo kati ya Tom na Danieli iliyoko katika kitabu cha mwanafunzi.

Uliza: Je! ni kijana yupi aliyelewa maana ya kweli ya kanisa, Tom au Danieli? Ndiyo, Tom ndiye aliyelewa hasa tafsiri ya kanisa. (Wape wanafunzi kadhaa nafasi ya kuweza kueleza maana ya kanisa.)

Uliza: Yesu alifikiria nini kuhusu kanisa? (Ngojea majibu.)

Sema: Tunaweza kupata kile ambacho Yesu alifikiria kuhusu kanisa na jinsi alivyolipenda, tunaposoma kifungu chetu cha kukumbuka. (Huu ndio wakati mzuri wa kufundisha kifungu cha kukumbuka.)

Uliza: Je! unafikiri Yesu alikuwa akizungumza juu ya kanisa lipi katika kifungu hiki, jengo au watu? (Waambie wanafunzi waiangalie picha ya jengo na picha ya kundi la watu iliyoko katika somo lao.)

Sema: Hata ingawa tunaita mahali pale tunapokutanikia kwa kuabudu kuwa ni "kanisa", hilo ni jengo tu. Kanisa la kweli ni wale watu ambao wamempokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao. Huwa ni wale waliobatizwa. Nao wote huwa sasa sehemu ya mwili wa Kristo, yaani kanisa.

Waambie wanafunzi wawili wasome 1 Wakorintho 12:12-13 na 12:20-27.

Mwambie mwanafunzi mmoja asimame mbele ya kanisa. Waonyeshe sehemu mbalimbali za mwili na uwaambie wanafunzi hao waseme majina yake wakati unapowaonyesha.

Uliza: Je! kwa nini Mungu alitumbua na sehemu tofauti za mwili? Je! kila sehemu inafanya kazi moja sawa na ile nyingine? Je! mwili unaweza kufanya kazi ile unaopaswa kufanya iwapo sehemu moja au mbili hazipo? (Tumia muda mwingi kwa kujadiliana majibu ya maswali haya.)

Sema: Washiriki wa kanisa wana kazi ya kufanya, jinsi sehemu zote za mwili zilizvyo za muhimu. Mungu anawahitaji watu wote wa kanisa, wazee, vijana na hata watoto. Yeye humtegemea mchungaji, kiongozi wa nyimbo, mashemasi na waalimu wa Shule ya Jumapili. Watu hawa ni wamuhimu kwa sababu wana-waongoza wengine katika kusifu,

kuabudu na kumtumikia Mungu. Wale wengine wanaobakia ni wamuhimu pia. Mungu anawahitaji na anawatarajia wamfanyie kazi. Ni lazima wote wafanye kazi pamoja kwa kushiriki na wenzao habari za Injili iwapo kanisa hili linataka kutekeleza kile ambacho Kristo alinuia kifanywe. Ni lazima wafanye kazi pamoja katika kuwasaidia Wakristo wapya ili wakue.

Uliza: Je! Unaweza kufanya nini ili umtumikie Mungu na kulisaidia kanisa? (Baadhi ya majibu yanaweza kuwa: kuimba, kuwasomea wengine Biblia, kuwatembelea wengine, kumpelekea mgonjwa chakula, kuwatunza watoto ili wazazi wao waende kuhudhuria mikutano, kupanga viti, kusaidia katika kufanya usafi kanisani, kukata nyasi, na kadhalika.)

Sema: Mungu anatumia tufanye kazi. Anatumia pia tufanye kazi pamoja. Inaweza kumchukua mchwa mmoja miaka mingi kuweza kujenga kichuguu wakati afanyapo kazi ya kujenga peke yake. Lakini mchwa wengi wanaweza kujenga kichuguu kwa haraka wafanyapo kazi pamoja.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Mathayo 16:15-18.

Sema: Yesu alisema kwamba kanisa lake lingekuwapo milele wala halingeweza kuharibiwa na cho chote. Maji, moto, upepo au wanyama wa mwitu wanaweza kuharibu jengo la kanisa lililojengwa kwa mbao au mawe, lakini hakuna kitu kiwezacho kudhuru kanisa, yaani waamini. Hata ingawa Wakristo wanawaza kuuliwa au kufa, wao wataendelea kuishi na

Yesu huko mbinguni. Yale mema waliyofanya wakiwa duniani yataendelea kuwavutia wengine.

KAZI YA KUFANYA

Wasaidie wanafunzi wako kufanya kazi iliyoko vitabuni mwao iwapo hawajaifanya. Rudia majibu yao ili uhakikishe kwamba yako sawa.

Weka alama (✓) kando ya jibu sahihi.

Kanisa ni:

— jengo tu.

✓ kundi la watu ambao wana-abudu na kumtumikia Mungu.

— hufunguliwa tu wakati wa Jumapili.

Mungu anawataka na anawatarajia watu wa umri wote kumsaidia katika kanisa. Piga mstari chini ya yale uwezayo kufanya ili umsaidie Mungu. Nile mahindi jinsi niwezavyo. Nisomee Biblia mtu ambaye hawezi kusoma. Nimpelekee mgonjwa chakula. Nimchokoze dada au ndugu yangu mdogo. Nikusanye sadaka. Nipande maua kuzunguka kanisa.

Chora mviringo kwenye vitu ambavyo ni _____ ya kanisa. Mbwa, gari, Biblia, mhubifi, pesa, watu.

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo:

1. "Kwa maana katika Roho Mmoja sisi sote tulibalizwa kuwa mwili mmoja..." (1 Wakorintho 12:13a).
2. Kanisa ni waamini au watu.

3. "Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja." (1 Wakorintho 12:20)

4. Yule anayezungumza katika Mathayo 16:16 ni Simoni Petro.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...kama Kristo naye alivyo-lipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25b).

Yesu alilipenda sana kanisa hata akafa kwa ajili yake. Tunapaswa kupenda kanisa na tuwe tayari kutumika na kuwasaidia wenzetu jinsi tuwezavyo.

WAKATI WA MWISHO

Tazama tena kusudi lako la kufundisha. Je! Unafikiri kwamba wanafunzi wameelewa maana na

kusudi la kanisa? Je! Unafikiri kwamba wako tayari kujitoa kwa kuabudu na kulitumikia kanisa?

Wape nafasi ya kuweza kuuliza maswali yo yote waliyonayo. Pengine utataka kutumia dakika chache kwa kurudia majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je! kanisa ni nini?
2. Je! Mungu anawataka watu wa umri wa wote walio washiriki wa kanisa wafanye nini?
3. Je! Unaweza kufanya nini ili utumike kanisani?

Omba kwamba wewe na wanafunzi wako mtaweza kutambua nafasi na njia za kumtumikia Mungu kanisani. Mshukuru Mungu kwa kuwapatia kanisa.

SURA YA PILI

JE! KANISA LIMEKUAJE?

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 28:18-20; Matendo 8:1-4

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wanafunzi wa kanisa lako wanaweza kufikiria machache sana juu ya kanisa. Pengine hawajui jinsi Injili ilivyoenea katika nchi nyingi za ulimwengu tangu siku ile ambapo Yesu alianzisha kanisa.

Unapofundisha somo hili, wasaidie wanafunzi kuelewa kwamba Mungu amewatumia watu mbalimbali katika kuhubiri Injili. Somo hili linatueleza juu ya watu watatu waliotumiwa, nao ni Paulo, mmojawapo wa wamisheni wa kwanza wa kanisa, Filipo, mmisheni wa kwanza aliyeweza kumshuhudia Mwafrika, na, David Livingstone, mmisheni wa karne hii aliyeishi Afrika kwa muda wa miaka mingi.

Wasaidie wanafunzi nao kuelewa kwamba Roho Mtakatifu humsaidia Mkristo kuweza kushuhudia wengine. Yeye ndiye aliyempa Paulo, Filipo, na David Livingstone uwezo wa kusafiri safari ndefu na kuwaeleza watu wote kuhusu upendo wa Mungu.

Tilia mkazo kwamba Mkristo ana wajibu wa kuwaambia wengine habari za Yesu Kristo hata ingawa yeye si mhubiri au mmisheni kama Paulo. Roho Mtakatifu atawawezesha Wakristo wa sasa jinsi alivyowasaidia Wakristo wa mwanzo.

Eleza kwamba kanisa limekua kutoka kwa watu wachache hadi kwa mamilioni ya watu kwa sababu baadhi ya Wakristo wameelewa na kutii agizo la Yesu lililoko katika Mathayo 28:18-20.

Soma maandiko. Maneno yaliyoko katika Mathayo 28:18-20 yanajulikana sana na Wakristo wengi. Yesu alikutana na wanafunzi wake kabla ya kwenda mbinguni. Aliwaambia yale ambayo walipaswa kufanya wakati ambapo atakuwa hayupo. Aliwatuma kwenda kila mahali wakiwafanya watu wote kuwa wanafunzi wake, wakiwabatiza na kuwafundisha. Maagizo haya hayakuwahusu tu wale kumi na mmoja waliokuwa pamoja na Yesu siku hiyo. Yalihusu Wakristo wote na mahali po pote walipo.

Hivi ndivyo kanisa linavyokua. Juhudi hii inaitwa "umisheni." Kanisa litakuwa dhaifu na halitakuwa iwapo haliendi kuwavuta watu na kushiriki Habari Njema na wengine.

Habari za kututia moyo zilizoko katika vifungu hivi ni kwamba Wakristo hawafanyi kazi hii peke yao. Roho Mtakatifu yupo ili kuwawezesha Wakristo kuwashuhudia wale ambao hawajui kwamba Mungu alimtura Mwanawe ili kuookoa ulimwengu.

Soma Matendo 8:1-4. Soma sura yote ya Matendo 8. Vifungu hivi vinaonyesha jinsi kanisa lilivyo-tawanyika na kuwaendea watu wa

mbali. Wakristo walihama na kwenda kuishi katika sehemu mbalimbali walipoanza kuteswa. Waliwapelekea injili watu wa sehemu hizo. Wayahudi hawakuwa wakiwafikiria Wasamaria kwa muda wa miaka mingi, lakini sasa tunasoma kwamba Filipo alikuwa Samaria akiwahubiria watu wa huko habari za Kristo. Roho Mtakatifu alikuwa akimsaidia Filipo kuwashuhudia wale watu ambao walikuwa maadui wa watu wao. Roho huyo huyo alimwongoza Filipo kuweza kumwelezea Mwethiopia habari za Injili. Tunaambiwa katika kifungu cha 26 hadi 40 katika sura hii jinsi Filipo alivyoenda Gaza ambako alikutana na Mwethiopia na akamwambia habari za Yesu, Masihi.

Wakati huo huo, Sauli alikuwa akiwatesa Wakristo, lakini tunasoma jinsi alivyoongoka katika sura ya 9 ya Matendo. Roho Mtakatifu alifanya kazi katika moyo wa Sauli hata siku moja alimsikia Yesu akisema naye alipokuwa akielekea Dameski kwenda kuwatesa Wakristo. Sauli, ambaye alipewa jina la Paulo, alibadilishwa kabisa na akawa mmisheni mkuu wa kanisa.

KUSUDI LA SOMO HILI

Ki sasaidia wanafunzi kuweza kuelewa jinsi kanisa lilivyokuwa na wajibu wao wa sasa katika kulisaidia kanisa kukua.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Tutasikiliza leo kipindi cha redio. Msimulizi atahojiana na wamisheni watatu wakuu. Hebu tusikilize kwa makini wakati watu

hawa wanavyosema jinsi Mungu alivyowatumia kwa kulisaidia kanisa kukua. (Mwambie mwanafunzi mmoja asome sehemu ya MSIMULIZI na wale wengine watatu wasome sehemu ya PAULO, FILIPO na DAVID LIVINGSTONE.)

Waambie wanafunzi hao wafungue kitabu cha Mathayo 28:16-20 na umwambie mmoja wao asome vifungu hivi.

Uliza: Je! Yesu aliwaachia wanafunzi wangapi kazi ya kueneza Injili alipoenda mbinguni? (Siku hiyo alikuwa na wanafunzi kumi na mmoja kando ya mlima.)

Sema: Siku hizi kuna mamilioni ya Wakristo ulimwenguni kwote. Kanisa limekua kwa sababu baadhi ya wafuasi wa Yesu wamekuwa waaminifu kwa kuwashuhudia wengine na waliani msaada wa Roho Mtakatifu.

Wafundishe kifungu cha kuku- mbuka, Matendo 1:8, na mjadiliane jinsi Roho Mtakatifu alivyolisaidia kanisa kukua.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Matendo 8:1-4. Tumia maelezo yaliyoko katika sehemu ya KUJIANDAA KUFUNDISHA ili uweze kueleza kilichokua kikiendelea kanisani.

Uliza: Je! mnafikiri Mungu aliwezaje kuwatumia Filipo, Paulo na David Livingstone ili kusaidia kanisa lake kukua? (Majibu yanaweza kuwa: Walitaka wawe waaminifu kwa agizo la Yesu la kuhubiri Injili, walimsikia

Mungu akiwaita kupitia kwa Roho wake ili wawaambie wengine habari za Kristo; walisaidiwa na Roho Mtakatifu kuweza kushuhudia ambapo hawangeweza, na kadhalika.)


Uliza: Je! Kunao watu ulimwenguni siku hizi ambao hawajui habari za upendo wa Mungu? (Eleza kwamba kunao wengi ambao hawajawahi kusikia habari za Injili. Ni lazima watu tofauti wapatao 750,000 waweze kushiriki habari za Injili kila siku ili kila mmoja aweze kusikia habari hii tufikiapo mwaka wa 2000. Hesabu hii imetolewa na mwalimu mmoja wa Kikristo wa huko Amerika aitwaye Bw. Avery Willis.)

Jadiliana na wanafunzi kuhusu wajibu wao wa kulisaidia kanisa kuweza kukua.

Wasaidie wanafunzi hao ili wamalize sehemu yao ya KAZI YA KUFANYA iwapo hawajamaliza.

KAZI YA KUFANYA

Unganisha namba zifuatazo, kuanzia 1 hadi 2 na 3 na endelea hadi 24 ili uone kile kitu ambacho Mwethiopia alikuwa akisoma wakati Filipo alipomwona.



Sentensi mbili kati ya hizi zifuatazo ni za kweli na moja si ya kweli. Weka alama (✓) kando ya zile zilizo za kweli na ukate kwa msitari sentensi ile ambayo si ya kweli.

☒ Paulo alikuwa akiitwa zamani Saulo.

☐ Paulo aliwapenda Wakristo.

☒ Paulo alipofuka alipokuwa njiani akielekea Dameski.

Uliwasikia wamisheni watatu wakizungumza katika kipindi cha radio. Andika majina ya wale wawili ambao waliwaelezea watu wa Afrika habari za Injili.

1. Filipo

2. David Livingstone

Weka alama (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

Mmisheni ni:

—mwuzaji wa samaki.

✓yule anayewaambia wengine habari za Mungu.

—yule anayewatukana Wakristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

Mungu anatutarajia tuwe mashahidi wake na tuwaambie wengine habari zake. Alijua kwamba hatungeweza kushuhudia bila usaidizi

wake, kwa hivyo alitutumia Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu amekuwa pamoja na Wakristo tangu Yesu alipoenda mbinguni. Nguvu zake ambazo zinafanya kazi katika wafuasi wa Yesu zimewezesha kanisa kukua. Yungali anawapa Wakristo uwezo wanapoendelea kuwaambia wengine Habari Njema za Yesu Kristo.

WAKATI WA MWISHO

Funga kwa maombi. Mwambie kila mwanafunzi ambaye atafanya hivyo amshukuru Mungu kwa ajili ya kanisa. Mwambie aweze kusaidia kanisa kwa kuwashuhudia wale waliopotea katika ulimwengu huu wa sasa.

SURA YA TATU

UJUMBE MKUU WA KANISA

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 4:5-12

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! Wanaelewa kile kilichomaanishwa katika Maandiko yanaposema kwamba Yesu ni jiwe kuu la pembeni la kanisa? Je! wanajua ujumbe wa kanisa ni upi? Baadhi ya watoto hujiunga na kanisa na kubatizwa wakiwa wangali vijana sana. Kwa hivyo unapofundisha somo hili utapata nafasi nzuri ya kuweza kuwasaidia kuelewa mengi zaidi kuhusu kanisa na ujumbe wake.

Unaweza pia kuwasaidia wanafunzi wako ambao ni Wakristo kuelewa wajibu wao wa kushiriki ujumbe huu na wale ambao si Wakristo. Petro na Yohana walishikwa kwa sababu ya kuhubiri na kuponya. Lakini kitendo hiki hakikuwazuia kumdhihirisha Yesu kuwa ndiye njia ya pekee ya kupata wokovu. Wanafunzi wako hawapaswi kuhubiri ili washuhudie, lakini unaweza kuwasaidia kugundia njia ambazo wanaweza kutumia kwa kushiriki na wenzao ujumbe wa Yesu Kristo.

Maandiko ya somo hili, yaani Matendo 4:5-12, yanaeleza kupelekwa kwa Petro na Yohana mbele ya wakubwa na wazee na waandishi. Kundi hili la watawala ndilo lilikuwa na mamlaka makuu juu ya Wayahudi. Petro na Yohana walikuwa wamekamatwa wakiwa hekaluni kwa kumponya kiwete mmoja na kwa

kuhubiri. Jamaa hii ya watawala wakuu ilikuwa kundi la uwezo mkubwa. Petro na Yohana walikuwa na shida kubwa. Kifungu cha 5 na 6 kinaorodhesha majina ya maafisa wa Kiyahudi ambao walikuwepo wakati wa hukumu. Hii inaonyesha kwamba wote walivutiwa na mitume hawa wawili na hata yale waliyokuwa wamefanya. Karibu kila mtu aliye mashuhuri alikuwepo. Kwa hivyo, jambo hili linatuonyesha kwamba kanisa la mwanzo lilikuwa likiyagusa maisha ya watu wengi wa Yerusalemu.

Petro na Yohana waliwekwa katikati ya wale wote waliomshtaki. Pengine ile jamaa ya watawala wakuu ilikuwa imekaa katika mfano wa nusu mviringo, wakiwaangalia mitume hawa wawili.

Hakimu akawauliza, “Kwa nguvu gani na kwa jina la nani ninyi mmefanya haya?” Petro na Yohana walijua kwamba wangepadhibiwa vikali sana iwapo wangewaambia ukweli. Lakini wao walikuwa wamejitoe kwa Yesu. Hawakuogopa cho chote, hata waliweza kushuhudia kwa ujasiri juu ya nguvu za Yesu. Ujasiri huu ulitokana na kujazwa kwa Roho Mtakatifu.

Madai ya Petro yaliyoko katika kifungu cha 9 hadi 12 ni ya muhimu sana wakati Wakristo wa sasa wanapojaribu kuelewa maana ya kweli ya ujumbe wa kanisa. Kifungu cha 10 kinasema kwamba Mungu alimfufua

Yesu kutoka kwa wafu. Huyu ndiye Yesu yule yule ambaye alisulibiwa na Wayahudi. Petro alisema kwamba kiwete huyu ameponywa kwa nguvu za Yesu.

Petro katika kifungu cha 11 alisema kwamba viongozi wa Kiyahudi walikuwa kama wajenzi wa taifa la Israeli. Nao kama wajenzi, walikuwa wamekataa "jiwe" ambalo halingefaa katika mpango wao wa ujenzi. Hatimaye Petro anasema kwamba Yesu ndiye jiwe kuu la pembeni la Israeli ya kweli, walio watu wa Mungu, yaani kanisa. Jiwe la pembeni ndilo jiwe la muhimu sana katika jengo. Maisha ya Yesu na ujumbe wake ndio ujumbe mkuu wa kanisa.

Kiini cha madai ya Petro ni kifungu cha 12. Alisema kwamba Yesu ndiye njia ya pekee ya wokovu. Utaona kwamba Petro alitumia maneno yale yale yaliyotumiwa na jamaa ya watawala wakuu wakati wa kuuliza swali lao. Ni kwa sababu ya Yesu na ni katika jina lake tu ambapo wokovu unaweza kupatikana. Kumbuka kwamba Petro alikuwa akisema na watu waliodai kwamba njia ya pekee ambayo mtu angekuwa na ushirika na Mungu ilikuwa ni kwa kutii sheria na mafundisho yote ya Kiyahudi. Haikosi kwamba watu hawa waliokuwa wakimsikiliza walishangazwa sana na habari njema hii ya Petro ihusuyo wokovu kupitia kwa yule ambaye walikuwa wamemsulibisha.

Huu ungali ujumbe wa kanisa. Mtu hawezi kuwa na ushirika mwema na Mungu kwa kuwa na imani katika Yesu Kristo ambaye alifia dhambi

zake. Anaweza kufurahia uzima wa milele kwa sababu Yesu alifufuliwa katika wafu na huwawezesha wale waliokufa katika dhambi kupata mimba mapya.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuelewa na kueleza kwa maneno yao wenyewe ujumbe mkuu wa kanisa.

KULIFUNDISHA SOMO

Wachague wanafunzi wanne watakao soma sehemu ya Anasi, Kayafa, Iskanda na Petro katika mchezo ulioko katika kitabu cha mwanafunzi. Watie moyo wa kuweza kuuiga na waongee jinsi wanavyo-fikiria kwamba watu hawa wangeongea.

Gundua yale Biblia isemayo. Waambie wanafunzi hao wafungue Biblia zao katika Matendo 4.

Sema: Petro na Yohana walikuwa wamepelekwa mbele ya wakubwa na wazee na waandishi ili wahukumiwe.

Uliza: Je! Wakubwa na wazee na waandishi walikuwa akina nani? (Hili lilikuwa kundi la watawala wenye mamlaka makubwa sana kati ya Wayahudi.)

Uliza: Je! Kwa nini Petro na Yohana walipelekwa mbele ya wakuu hawa ili wahukumiwe? (Walikuwa wamemponya kiwete mmoja aliyekuwa akikaa karibu na lango la Hekalu, Matendo 3:6-8, nao walikuwa wakifundisha kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu, Matendo 4:1-2)

Sema: Kifungu cha 4 kinatwambia kwamba watu elfu tano walisikia mahubiri ya mitume hao na wakaamini yote waliyosikia kuhusu Yesu. Kanisa la mwanzo lilikuwa linakua. Watu wengi walikuwa wanaanza kumfuata Yesu. Ilionekana kama kwamba viongozi wa kidini wangepurahi sana, lakini badala yake walikasisirika sana.

Uliza: Je! mnafikiri walikasisirika kwa nini? (Ngojia majibu)

Sema: Viongozi wa kidini waliamini kwamba njia pekee ambayo mtu anaweza kuokolewa kwayo ni kupitia kwa sheria na mafundisho ya kidini. Hawakumkubali Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu ambaye alifufuka katika wafu baada ya kusuliwa.

Sema: Sasa angalieni katika kifungu cha 10 na mwone ni nani alimpa Petro na Yohana uwezo wa kufundisha na kuhubiri. (Yesu Kristo)

Sema: Petro na Yohana walijua kwamba wale watu wa kotini hawangepurahia yale ambayo walikuwa wanasema kuhusu Yesu. Walijua kwamba viongozi hawa wangewapiga na kuwafunga tena gerehani.

Uliza: JE! Petro na Yohana waliogopa -kuendelea kusema ukweli juu ya Yesu na kanisa? (La)

Sema: Semeni kifungu cha 8 na mwone sababu iliyowafanya wasiaye. (Walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu.)

Waambie wanafunzi hao wasome kimoyomoyo kifungu cha 11 na 12.

Sasa kisome kwa sauti baada ya wao kumaliza.

Uliza: Je! ni mambo gani mawili muhimu ambayo Petro alizungumzia katika vifungu hivi kuhusu Yesu? (Yesu alikuwa ndiye "jiwe" lililokataliwa na viongozi wa Kiyahudi na hakuna njia nyingine ya kupata wokovu ili kupitia kwa Yesu Kristo.)

Sema: Jiwe la pembeni ndio jiwe muhimu sana katika jengo lo lote. Hili ndilo jiwe la kwanza ambalo huwekwa na wajenzi. Petro alisema kwamba viongozi wa Kiyahudi walikuwa sawa na wajenzi wa taifa la Israeli. Nao kama wajenzi, walikuwa wamekataa Yesu, aliye jiwe la pembeni, kwa sababu hakufaa katika mpango wao wa ujenzi. Viongozi wa kidini walikuwa na mpango wao wenyewe uhusio umuhimu wa sheria na mafundisho ya kiyahudi. Walimkataa Yesu kama Mwana wa Mungu, ambaye ndiye tu angewaokoa kutoka kwa dhambi zao. Lakini sasa Yesu alikuwa akisema kupitia kwa mitume wake kwamba Yesu ndiye jiwe la kweli la pembeni, msingi wa Israeli mpya, yaani kanisa. (Pengine utataka kutumia picha ya jengo la mawe kuelezea maana ya "jiwe la pembeni." Tilia mkazo kwamba kanisa halisimami kamwe iwapo litajengwa juu ya kitu au mtu mwingine badala ya Yesu Kristo.

Jadilianeni kile ambacho Petro alimaanisha aliposema kwamba, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote..." kifungu cha 12.

Uliza: Je! ni njia zipi zingine ambazo watu hutumia ili wamfikie Mungu? (Kupitia kwa viongozi wa kidini, kwa kutenda mema, na kadhalika.)

Sema: Hakuna njia yo yote iwezayo kukuokoa ila kupitia kwa Yesu Kristo. Kanisa limejengwa juu ya Yesu Kristo. Yesu ndiye aliyeanzisha kanisa. Aliwaachia wafuasi wake kazi ya kanisa. Ni wajibu wa wafuasi hawa kuwaambia wengine jinsi Yesu alivyokuja duniani, akasulibiwa na hatimaye akafufuka tena. Ujumbe wa kanisa ni kwamba dhambi hututenganisha na Mungu. Huwa tunafaa tufe tunapotenda dhambi, lakini Yesu anatupenda sana hata amekufa badala yetu. Hutupa uzima wa milele badala ya mauti. Hakuna ye yote awezaye kutuokoa. Huu ndio ujumbe wa kanisa ambao Petro alihubiri mbele ya wakubwa na ya wazee na waandishi wa Kiyahudi.

Someni pamoja Matendo 4:12.

Mpe kila mwanafunzi kalamu na uwaambie wajibu maswali yote yaliyoko katika sehemu ya "Kazi ya Kufanya." Jadilianeni majibu hayo baada ya wao kumaliza. Hakikisha kwamba kila mwanafunzi anaelewa ujumbe wa kanisa. Mwambie kila mwanafunzi asome kwa sauti yale aliyoandika kuhusu ujumbe wa kanisa.

KAZI YA KUFANYA

Piga mstari chini ya sentensi za kweli zihusuzo Petro.

Petro alimponya kiwete yule ili aweze kujulikana sana.

Aliogopa kuwaambia wazee, wakubwa na waandishi wa Kiyahudi habari za Yesu.


Petro alimtegemea Yesu kwa kumpa uwezo wa kumwezesha kuhubiri na kuponya.

Alisema kwamba wokovu unapati-kana kwa Yesu pekee.

Petro alihubiri kwamba Yesu ndiye jiwe pekee la pembeni la kanisa.

Chora mviringo juu ya jibu lililo sahihi:

Petro alimponya kiwete yule katika jina la:



Kanisa



Mfalme

Je! ni nani kichwa cha kanisa?
Weka alama (✓) kando ya jibu lililo sahihi:

___ wanafunzi kumi na wawili

___ mchungaji wangu

✓ Yesu Kristo

___ washiriki wa kanisa

Andika katika nafasi ifuatayo yale uelewao kuwa ndiyo ujumbe wa kanisa (Tazama Matendo 4:11-12).

Jibu la mwanafunzi linapaswa kueleza kwamba ni katika Yesu tu ambapo mtu ataweza kuokolewa.

Ikiwa wewe u Mkristo na mshiriki wa kanisa, taja njia ambazo unaweza kushiriki ujumbe huu na wenzako.

(Ngojea jibu la mwanafunzi)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo 4:12).

Wasaidie wanafunzi wajifunze kwa moyo kifungu hiki iwapo hawajafanya

hivyo. Pengine mashindano ya aina fulani yatawafanya wanafunzi hawa waweze kujifunza kwa moyo kifungu cha kila somo.

Hebu fikiria tena juu ya kusudi la somo hili. Je! mafundisho yako yamewawezesha wanafunzi hao kueleza katika maneno yao wenyewe juu ya ujumbe mkuu wa kanisa? Je! Iwapo waweza kueleza, basi ni mabadiliko gani ambayo yanaweza kutokea maishani mwao? Darasa lako ni tofauti sana na darasa lingine lo lote. Unajua mahitaji ya wanafunzi wako. Je! Somo hili linawezaje kugusa maisha yao?

WAKATI WA MWISHO

Uliza maswali ambayo yatakusaidia kujua kama wanafunzi wako wanaelewa ujumbe wa kanisa. Wahimiza kufanya sehemu yao ya kushiriki na wenzao ujumbe huu, ambao hawajui mtu anaweza kuokolewa tu kupitia kwa Yesu Kristo. Funga kwa maombi ya kuwataka wawe washiriki wema wa kanisa.

JE! Naweza kuwa mshiriki wa kanisa?

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 2:36-43

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! ni wanafunzi wangapi wa darasa lako ambao wameamua kumfuata Yesu, ambao wamebatizwa na ni washiriki wa kanisa? Je! wanafunzi wote wameelewa jinsi ya kuokolewa?

Mara nyingi vijana hawajui maana hasa ya kuwa mshiriki wa kanisa. Somo hili litakupa nafasi ya kukazia kwamba ni lazima mtu aokoze kwanza kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa. Neno hili "kuokolewa" huwa linatumiwa bila ufahamu. Eleza maana ya neno hili ili wanafunzi waweze kulielewa.

Hakikisha kwamba wanafunzi wanaelewa kwamba ubatizo na kuwa mshiriki wa kanisa huja baada ya kuokolewa.

Pengine utataka kumwalika mchungaji wako kuja na kuzungumzia yale yahasuyo kuwa mshiriki wa kanisa.

Pengine utataka kuzungumza juu ya wokovu wako, ubatizo na jinsi ujisikiavyo kwa kuwa u mshiriki wa kanisa.

Soma sura yote ya pili ya kitabu cha Matendo. Mungu alikuwa ameahidi kuwapa wanafunzi wake msaidizi, yaani Roho Mtakatifu. Sura ya pili inatwambia kwamba aliweza kutimiza ahadi hii. Nguvu za Roho Mtakatifu

zilizimwezesha Petro kuhubiri kwa uwezo mkuu. Petro alikuwa akiwahubiria Wayahudi walioifuata sana dini yao ambao walikuwa wamekusanyika wakati wa sherehe. Alikuwa akijaribu kuwashawishi kwamba Yesu alikuwa Masihi ambaye walikuwa wakimngojea. Petro alimalizia ujumbe wake katika kifungu cha 36 kwa kukazia kwamba Yesu Kristo ndiye Masihi.

Mahubiri ya Petro yaliwagusa sana wale waliokuwa wakisikiliza. Kifungu cha 37 kinasema kwamba "walichomwa mioyo yao" waliposikia habari hiyo. Hawakubisha wala kukataa yale ambayo Petro alisema. Wao waliuliza tu, "Tutendeje, ndugu zetu?"

Petro aliwajibu wazi, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu..." Baadhi ya watu wamebishana kuhusu maana ya maneno haya. Swali lenyewe lahusu hasa ubatizo baada ya kuokolewa. Je! Petro alikuwa akisema kwamba ni lazima mtu atubu na abatizwe ndipo asamehewe dhambi zake? Au alikuwa akisema kwamba analazimishwa tu kutubu?

Neno "toba" ndilo la muhimu sana. Linamaanisha kubadili nia yako; na kubadili mwenendo wako wa maisha yako. Maana ya kifungu hiki ni kwamba mtu ataweza kubatizwa tu baada ya kutubu.

Je! Ni nini maana ya “Mpate ondoleo la dhambi?” Neno muhimu hapa ni “mpate”. Neno hili linamaanisha kwamba mtu hubatizwa kwa sababu ya au kwa ajili ya msamaha wa dhambi ambao ameupata kutokana na kutubu. Maelezo haya yanaelekeana na mafundisho yote ya Agano Jipya yahusuyo wokovu.

Petro hakuwa akiwaambia watu kwamba wanapaswa kubatizwa ili waokolewe. Alikuwa akisema kwamba wanapaswa kutubu ili wapate wokovu. Hatimaye watapaswa kubatizwa kwa sababu ya wokovu. Ubatizo huonyesha wazi kile ambacho kimetokea maishani mwa mtu fulani.

Petro aliwaambia watu hao kwamba wangepata “kipawa cha Roho Mtakatifu” baada ya kuokolewa. Kipawa hiki ni Roho Mtakatifu ambaye angewajia waamini wote, wala si wachache tu.

Petro alihubiri na uwezo mkubwa hata watu wengi wakaweza kuokolewa. Watu wapatao elfu tatu walibatizwa na wakawa sehemu ya ushirika wa kanisa.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuweza kuelewa maana ya “kuokolewa” na kwamba ye yote atakaye kuwa mshiriki wa kanisa anapaswa kubatizwa baada ya kuokolewa.

KULIFUNDISHA SOMO

Watangazie kwamba leo mtakuwa na mchezo wa kuigiza uhusuo msichana aitwaye Hana. Hana anataka kujiunga na kanisa, lakini

haelewi maana ya “kijiunga na kanisa”. Waambie washiriki wawili wa darasa lako wasome sehemu ya Hana na mwalimu.

Uliza: “Je! Kwa nini Hana alitaka kujiunga na kanisa? (Alitaka kuwa mshiriki wa kanisa kwa sababu marafiki wake wote walikuwa washiriki. Hakuelewa maana ya kuwa mshiriki wa kanisa au kile kinacho hitajika kufanywa ili uwe mshiriki wa kanisa.

Uliza: Je! ni sababu zingine zipi ambazo zinaweza kuwafanya watu watake kuwa washiriki wa kanisa? (Wape wanafunzi hao muda wa kuweza kujadiliana juu ya majibu yake. Baadhi ya sababu zaweza kuwa, kwa sababu jamaa au marafiki zao ni washiriki wa kanisa hilo. Pengine wanataka kujua kile kifanyikacho kanisani, na wanataka wawe sehemu yake. Pengine wale walio wazima watajisikia kwamba ushirika wa kanisa utawasaidia kukubaliwa katika jamii yao.)

Gundua yale Biblia isemayo. Waambie wanafunzi hao wasome kwa sauti Matendo 2:36-42. Eleza msingi wa vifungu hivi.

(Tazama sehemu chini ya KU-JIANDAA KUFUNDISHA. Tumia maelezo haya ili yakusaidie kueleza maana ya “kutubu”).

Sema: Ni lazima mtu asikitikie dhambi zake kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa. Hataki tena kufuata njia yake mwenyewe, bali anataka kubadili (kutubu) na kumfuata Yesu. (Unaweza

kueleza ukweli huu kwa kutembea ukielekea upande mmoja, halafu baadaye ugeuke na kwenda upande mwingine.)

Uliza: Je! Petro aliwaambiaje tu walipomwuliza jambo la kufanya? Soma kifungu cha 38.

Sema: Mungu humsamehe mtu anapotubu. Anaweza kupokea msamaha huu kupitia kwa Yesu Kristo aliyekufa kwa ajili ya dhambi zake. Mtu huanza kufikiria juu ya kujiunga na kanisa baada ya kumwamini Kristo ili amwokoe na kutaka kumpa nafasi ya kwanza katika maisha yake.

Uliza: Je! ni jambo lipi tena linalohitajika kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa? (Ubatizo)

Uliza: Je! Ubatizo humwoko mtu? (La, Yesu tu ndiye awezaye kuokoa)

Uliza: Sasa kwa nini ubatizo unahitajika kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa? (Ngojea majibu)

Eleza kwamba: Yesu alitupa mfano wa kubatizwa. Hakuwa amefanya dhambi, lakini alibatizwa ili kutuonyesha jinsi ya kufanya. Tunapobatizwa huwa tunaonyesha ul wengu kamba tumetubu dhambi zetu na tunamfuata Yesu. Tutajifunza mengi kuhusu maana ya ubatizo katika somo lifuatalo.

Uwe na uhakika kwamba wanafunzi hao wanaelewa maana ya "kuokoka" na ni lazima kwanza jambo hili lifanyike kabla ya mtu ye yote kuwa mshiriki wa kanisa.

Uliza: Je! Inamaanisha nini kuwa Mkristo? (Wape wanafunzi muda wa kufikiria juu ya swali hili na kuweza kujibu.)

Pengine utataka kutoa ushuhuda mfupi jinsi ulivyookoka, na kubatizwa na mwishowe ukawa mshiriki wa kanisa.

Mpe mchungaji wako muda wa kuwaambia wanafunzi hao juu ya ushirika wa kanisa iwapo ume-mwalika.

Wasaidie wanafunzi hao katika sehemu ya "kazi ya kufanya." Sahihisha majibu yao.

KAZI YA KUFANYA

Chora mstari katika sentensi ambayo si ya kweli.

~~Ubatizo ndiyo njia ya kuwa Mkristo.~~

Ubatizo huwaonyesha wengine kwamba umetubu dhambi zako na unataka kumfuata Yesu.

Mtu huwa Mkristo kabla hajabatizwa.

Andika vizuru maneno yafuatayo ili utambue kile ambacho hutokea maishani mwa mtu kabla ya kuwa mshiriki wa kanisa.

IN MAZILA ATUUB DHIBMA
KAEZ AN MIMWANIA SUYE
IIL AKOLOEWE (NI LAZIMA
ATUBU DHAMBI ZAKE NA
AMWAMINI YESU ILI
AOKOLEWE)

Je! Petro alisema kwamba wale wanaotubu watapokea nini? (Matendo 2:38b)

Kipawa cha Roho Mtakatifu

Chora katika nafasi ifuatayo picha ya mtu anayeuliza kuwa mshiriki wa kanisa au mtu anayebatizwa. Au, tafuta picha yo yote katika gazeti ihusuyo mtu anayeuliza kuwa mshiriki wa kanisa au mtu anayebatizwa. Shikamanisha picha hiyo katika nafasi ifuatayo.

huwa sasa ni sehemu ya mwili wa Kristo. Anahitaji msaada wa Wakristo wenzake. Kanisa litamsaidia kukua kama Mkristo. Kanisa litampa Mkristo huyu mpya nafasi ya kutumika.

Kujiunga na kanisa au kubatizwa hakuwezi kumwokoia mtu kutoka kwa dhambi zake. Ni imani tu katika Yesu ambayo inaweza kuokoa. Lakini wakati Wakristo wanaweza kusimama imara kama mashahidi wa ulimwengu wanapokutanika pamoja kama kanisa.

WAKATI WA MWISHO

Mshukuru Mungu kwa kutoa njia ya kuweza kuokolewa kwa kumwamini Kristo kama Mwokozi. Mshukuru kwa sababu tunaweza kumtumikia kupitia kwa kanisa lake.

Waombe wale ambao bado hawajaokoka.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Basi nanyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake” (1 Wakorintho 12:27).

Waongoze wanafunzi katika kujifunza kifungu cha kukumbuka. Mwambie kila mmoja kusema kifungu hicho, halafu uwaambie wote wakisema kwa pamoja.

Sema: Mtu anapaswa kuwa mshiriki wa kanisa baada ya kumpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wake. Yeye

SURA YA TANO

JE! UBATIZO UNAMAANISHA NINI?

MASOMO YA BIBLIA: Matendo 16:29-34; Warumi 6:1-4

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Somo la wanafunzi lina mazungumzo kati ya Samweli na mamake. Wanafunzi wako wengi wanaweza kuwa kama Samweli. Pengine kuna mambo mengi yahasuyo ubatizo ambayo hawaelewi. Nao wanataka kuyajua. Uwe tayari kujua maswali yao.

Unafaa kujihakikisha kwamba wanafunzi hao wanaelewa kwamba ubatizo hauwezi kumwokoza mtu yote. Ubatizo hauhitajiki ili mtu aokolewe, lakini unahitajika wakati wa kuwa mshiriki wa kanisa. Unahitajika kwa sababu Yesu aliwapa Wakristo mfano huo na akawaamuru wanafunzi wake wabatizwe. Ubatizo ni kama kuvaa vazi la Kikristo. Ni picha ya kudhihirisha kile kilichotokea katika maisha ya mtu huyo.

Makundi mengi yanawabatiza watoto wachanga. Kwa hivyo utapaswa kutilia mkazo kwamba kanisa la Agano Jipya liliwabatiza tu wale ambao walikuwa wamemkiri Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao. Wakristo Wabatisti hufuata mtindo huu wa Agano Jipya.

Uwe tayari kueleza wazi maana au ishara ya ubatizo. Pengine utapanga kuwapeleka wanafunzi wako mahali ambapo kanisa lako huwabatiza watu iwapo pako karibu na kanisa. Mkishafika hapo, sasa unaweza kuzungumzia maana ya ubatizo.

Kuna mifano mingi jinsi kanisa la mwanzo lilivyowabatiza Wakristo wapya. Mfano mmoja unapatikana katika Maandiko ya somo letu la leo ambalo lapatikana katika Matendo. Anza sasa kusoma Matendo 16:16 hadi mwisho wa sura hiyo.

Wakati Paulo na Sila walipofungwa katika jela huko Filipi, hawakukaa gereza ni wakijisikitikia. Bali walishuhudia imani yao kwa Mungu kwa kuomba na kuimba. Wafungwa wenzao waliwasikiliza. Ulipofika usiku wa manane, tetemeko kuu la arthi lililingisha msingi wa gereza lile hadi milango yake ikaweza kufunguka. Minyororo ambayo walikuwa amefungiwa iliweza kufunguka. Wakati mlinzi wa gereza alipoamka na kuona kilichokuwa kimefanyika, alikuwa na uhakika kwamba wafungwa hao wamekimbia. Hata alikuwa tayari kujua. Kulingana na sheria ya Warumi mlinzi alikuwa amejitoa pamoja na maisha yake kuwa ulinzi wa wafungwa. Paulo alimpazia mlinzi huyo sauti akimwambia kwamba asijidhuru mwenyewe kwa sababu wafungwa wote walikuwa wangali wako gereza ni.

Mlinzi yule aliingia kwa haraka mle gereza ni. Akawaona Paulo na Sila. Alianguka miguuni pa watu hawa wawili na akawauliza, "Bwana zangu yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" Walimwambia mlinzi huyo jambo la pekee linalohitajika kwa kupata wokovu. Ni lazima amwamini Bwana Yesu.

Mlinzi yule aliwakaribisha Paul na Sila nyumbani kwake na akawaosha majeraha yao. Paulo na Sila waliwashuhudia wote waliokuwa katika nyumba yake. Wote waliamini. Baadaye usiku huo wote waliokuwa wameamini walibatizwa. Nyumba yake yote ilikubaliwa kubatizwa kutokana na hatua moja ya imani iliyochukuliwa na yule mlinzi na jamaa yake.

Warumi 6:1-4, ambayo ni Maandiko mojawapo ya somo la leo, yanaeleza maana ya ubatizo. Ubatizo ni mfano wa kuonyesha kile kilichofanyika maishani mwa mtu. Vifungu hivi vinasema kwamba wakati mtu anapochovywa ndani ya maji, ni kama kuzikwa. Wakati anapotolewa ndani ya maji ni kama kufufuka kutoka kaburini. Ubatizo ni picha ya kufa na kufufuka. Mtu hufia aina fulani ya maisha na hufufuka akiwa katika maisha mengine mapya. Hufia maisha ya zamani ya dhambi na hufufuka akiwa katika maisha mapya ya neema.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwaongoza wanafunzi kuweza kuelewa maana ya ubatizo wa Agano Jipya.

KULIFUNDISHA SOMO

Mpe kila mwanafunzi kalamu na karatasi. Waambie waandike swali lo lote ambalo wanaweza kuwa nalo lihusulo ubatizo. Wahimize ili waweze kuuliza swali lo lote ambalo hawaelewi lihusulo ubatizo. Iwapo kuna kalamu na karatasi utapaswa kuwaambia wanafunzi hao waulize maswali yao huku ukiyaandika

ubaoni. Wasomee maswali hayo ambayo umeyaandika au uwaambie wanafunzi hao wasome maswali yao.

Sema: Ninyi ni kama yule kijana, Samweli, aliyetajwa katika hadithi yetu ya leo. Alikuwa na maswali mengi yahasuyo ubatizo. Hebu tuone kama ni sawa na haya yenu. (Soma hadithi hiyo au uwaambie wanafunzi wawili wasome sehemu hizo mbili, kati ya Samweli na mama yake. Linganisha maswali ya Samweli na yale ya wanafunzi baada ya kumaliza kusoma hadithi hiyo.)

Gundua yale Biblia isemayo. Sema: Agano Jipya linatuambia kuhusu mara nyingi ambapo watu walibatizwa. Mojawapo ya wakati kama huu umeandikwa katika Matendo 16.

Rudia tukio lililompata Paulo na Sila walipokuwa gerezeni na jinsi yule mlinzi na nyumba yake walivyo-okolewa. Uliza maswali na uwaambie wanafunzi hao kutafuta majibu yake.

Uliza: Je! ni nini kilichofanyika maishani mwa mlinzi yule na mwa jamaa yake kabla ya wao kubatizwa? (Walimwamini Yesu Kristo.)

Sema: Hebu sasa tutazame Warumi 6:1-4, ambayo inaeleza maana ya ubatizo. (Mnaweza kwenda na kuzungumza juu ya vifungu hivi mahali ambapo kanisa lenu hubatizia watu iwapo pako karibu na kanisa hilo. Mwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi.)

Uliza: Je! kunaye awezaye kueleza picha ionyeshwayo au mfano wa ubatizo? (Ngojea majibu. Hakikisha

kwamba mawazo yote yaliyoko katika aya ifuatayo yameelezwa kwa ukamilifu.)

Ubatizo ni “picha” ya kile kilichofanyika maishani mwa mtu. Vifungu hivi vinasema kwamba wakati mtu apochovywa ndani ya maji, ni kama kuzikwa. Wakati anapotoka ndani ya maji huwa mfano wa kufufuka kutoka kaburini. Ubatizo ni picha ya kufa na kufufuka. Mtu hufia aina moja ya maisha na kufufuka akiwa katika aina nyingine ya maisha mapya. Hufia maisha ya zamani ya dhambi na hufufuka akiwa katika maisha mapya ya neema.

Uliza: Je! mnafikiri ni kwa nini kanisa letu huhitaji ubatizo kabla ya mtu kuweza kuwa mshiriki wa kanisa? (Majibu yanaweza kuwa na wazo kwamba ubatizo ni ushuhuda kwa wengine kwamba mtu huyu sasa yuko tayari kuishi maisha mapya na yaliyo tofauti au kuonyesha kwamba kanisa letu linafuata yale yanayofundishwa katika Agano Jipya. Utapaswa pia kusema kwamba Yesu alimwambia Yohana ambatize hata ingawa hakuwa ametenda dhambi na kuhitajika kutubu dhambi zake ili abatizwe. Kwa kufanya hivyo, alikuwa kitu kimoja na wale waliohitaji kutubu. Baadaye, kabla Yesu hajarudi kwa Baba yake, aliwaamuru wafuasi wake kuhubiri, kufundisha na kubatiza.)

Mnapaswa sana mrudi darasani mwenu iwapo mlienda mahali pale ambapo kanisa lenu hubatiza washiriki wake. Wasaidie wanafunzi wako waweze kukamilisha sehemu yao ya “Kazi ya Kufanya.”

KAZI YA KUFANYA

Weka alama (✓) kando ya jibu lililo sahihi.

Yoshua alibatizwa

_____akiwa nyumbani.

_____karibu na mji.

✓ _____mtoni.

Chora mviringo kwenye jibu lililo-sahihi.

Yoshua alibatizwa na

mchawi

babu yake

mchungaji wake

shemasi

Jaza nafasi zilizo achwa za vifungu hivi:

1. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake...” (Warumi 6:4a)
2. “Hasha! sisi tuliofia dhambi tutaishiye tena katika dhambi?” (Warumi 6:2)
3. “Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?” (Warumi 6:3)

Taja majina ya watu wawili walioko katika Matendo 16:25 ambao walikuwa gerezani.

Paulo na Sila

Jibu swali lifuatalo:

Je! ni lazima mtu afanye nini kabla hajabatizwa?

Ni lazima amwamini Yesu Kristo
kama Bwana na Mwokozi wake.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**“Maana ninyi nyote mliobatizwa
katika Kristo mmemvaa Kristo”
(Wagalatia 3:27).**

Andika kila neno la kifungu cha kukumbuka kwenye vijikaratasi kabla ya kwenda darasani. Wape wanafunzi vijikaratasi hivi na uwaambie wajipange kulingana na jinsi maneno hayo yalivyo katika Biblia. Waambie wanafunzi hao warudie kifungu hiki mara nyingi.

Uliza: Je! mnafikiria kifungu hiki kina maanisha nini? (Ngojea majibu.)

Sema: Ni kwa njia ya imani tu ambapo tunafanywa wana wa Mungu.

Watu kama hawa huwa “wamebatizwa katika Kristo.” Huwa na ushirika na Kristo. Ushirika huu huonyeshwa au hudhihirishwa kupitia kwa agizo la ubatizo. Agizo ni sharti au amri ya Yesu ambayo ingali inafuatwa.

WAKATI WA MWISHO

Hakikisha kwamba umejibu maswali yote ambayo wanafunzi hawa wanayo yahusuyo ubatizo. Waambie kwamba watajifunza juu ya agizo lingine la kanisa katika somo lifuatalo, ambalo ni Chakula cha Bwana. Waambie watafute habari yo yote ihusuyo Chakula cha Bwana kabla ya wiki ijayo.

Funga kwa maombi.

SURA YA SITA

CHAKULA CHA BWANA

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 26:17-19, 26-28; 1 Wakorintho 11:23-29

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! ni wangapi wao ni Wakristo nao hushiriki katika Chakula cha Bwana? Je! wao huondoka mapema wakati wengine wanaposhiriki katika Chakula cha Bwana? Je! wanaelewa maana ya agizo hili la kanisa?

Majibu ya maswali haya yatakusaidia kujua kile ambacho utatilia mkazo unapofundisha somo hili.

Kuna Wakristo wengine ambao hawashiriki katika Chakula cha Bwana. Hii inaweza kuwa ni kwa sababu hawaelewi wala kujua umuhimu wake. Au, wanaweza kufikiria kwamba kunywa divai na kula mkate ni sawa na kula kiapo. Baadhi ya watu huamini kwamba hawawezi kushiriki katika chakula cha Bwana iwapo wao ni wagonjwa. Wengine hawawezi kuelewa kile Paulo alim. nisha alipozungumza juu ya kula Chakula cha Bwana isivyostahili. Hufikiria kwamba wanapaswa kuwa wakamilifu ili washiriki kwacho. Jaribu kuona iwapo mambo haya yanazusha matatizo katika kanisa lako.

Utapaswa wakati wa wiki kuandika kwenye karatasi na kwa herufi kubwa maana ya neno "Agizo." Andika

maana ifuatayo: Agizo ni sharti au amri ya Yesu ambayo ingali inafuatwa na kanisa. Utatumia karatasi hii unapozungumza juu ya ubatizo na Chakula cha Bwana kama aina ya maagizo ya kanisa.

Andika kifungu cha kukumbuka kwenye karatasi kubwa na pia kwa herufi kubwa. Sasa hata karatasi hii katika vijishehemu kumi visivyotoshana ili viwe kama fumbo. Vijishehemu hivi vitatumiwa ili kuwasaidia wanafunzi hao kujifunza kwa moyo kifungu hiki.

Soma Mathayo 26:17-19 na 26-28. Yesu alikuwa amekuja Yerusalemu kushiriki katika siku kuu ya Pasaka. Wanafunzi wake walitaka kujua matayarisho ambayo yamefanywa. Kulingana na mdandiko haya unaweza kuona kwamba Yesu alikuwa amefanya matayarisho yote.

Siku kuu ya pasaka ilisherehekewa ili kukumbuka jambo kuu lililotokea katika historia ya Waisraeli, wakati ambapo walikombolewa kutoka utumwani kule Misri. Yesu angeshiriki katika chakula hiki pamoja na wanafunzi.

Mara kwa mara Yesu alitumia mifano alipotaka kusema jambo katika njia ambayo wanafunzi wake hawangeweza kukosa kuelewa. Hivyo ndivyo alivyofanya wakati alivyokula chakula cha mwisho pamoja na wanafunzi wake. Sikukuu ya Pasaka

ilisherehekewa ili kukumbuka jinsi Waisraeli walivyokombolewa kutoka Misri. Yesu alikuja ili amkomboe mwanadamu kutoka kwa hofu na dhambi.

Mwana kondoo aliyechinjwa wakati wa Pasaka alikuwa kama mfano wa usalama. Ilikuwa damu ya mwana kondoo ambayo iliwaitea Waisraeli usalama wakati malaika wa mauti alipopita nchini humo. Yesu alikuwa akisema kuwa yeye ndiye mkombozi. Alikuwa kuwapa watu usalama wa milele.

Katika kifungu cha 28, Yesu amezungumza juu ya damu yake kuwa ni damu ya agano. Je! hii inamaanisha nini? Alikuwa akizungumzia mapatano au uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Uhusiano mpya kati ya Mungu na mwanadamu ungewezekana kwa sababu ya maisha na kifo cha Yesu. Uhusiano huu ungetegemea neema ya Mungu.

Sasa soma 1 Wakorintho 11:23-29. Paulo hakupendezwa na jinsi kanisa la Korintho lilivyoshiriki katika Chakula cha Bwana. Inaonekana kama kwamba hawakutilia maanani hasa maana ya kweli ya agizo hili. Walikuwa wakitumia wakati huu kama ule wa kufurahi na kula pamoja. Walikuwa wakiwakataza watu wengine wote isipokuwa wale waliokuwa katika kundi lao. Pengine wale matajiri walikuwa wakila chakula chote kabla maskini hawajafika. Hata baadhi yao walikunywa hadi wakalewa. Hii haikuwa njia ambayo walipaswa kushiriki katika Chakula cha Bwana, kwa hivyo Paulo alikuwa

akijaribu kuwasaidia Wakorintho kurekebisha makosa haya. (Tazama somo la wanafunzi ili uweze kujadiliana juu ya sikukuu ya upendo.)

Paulo alidhihirisha wazi siku ya kwanza ambayo kulikuwa na ushirika wa Chakula cha Bwana. Alisema kwamba, "...Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate..." (1 Wakorintho 11:23) Paulo aliendelea kueleza wazi akiorodhesha jinsi mambo yanavyofuatana. Ilikuwa ni kutii desturi ya Kiyahudi ya kutoa shukrani.

Yesu baada ya kumega mkate, alisema kwamba, "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu." (kifungu cha 24) Paulo aliwakumbusha Wakorintho maneno ya Bwana kwa ajili ya sababu maalum. Kulingana na Wayahudi, wakati huu wa Pasaka ulikuwa wakati wa kutilia mkazo hasa kukumbuka jinsi walivyoondoka Misri. Chakula cha Bwana kitilia mkazo hasa kukumbuka mtu (Yesu) wala si kitendo.

Mwamini anapomkumbuka Yesu, anapaswa hasa kukumbuka dhabihu ambayo Yesu alitoa kwa ajili ya wenye dhambi. Ukumbukaji wa Yesu unapaswa kumkumbusha mwamini juu ya kusuliwa na kufufuka kwake. Anapaswa kukumbuka uwezo wa Yesu wa kushinda mauti na kaburi. Vile Wayahudi wanavyokumbuka jinsi nguvu za Bwana zilivyowatoa Misri, ndivyo hivyo Wakristo wanavyokumbuka jinsi nguvu za Bwana zilivyowatoa Misri, ndivyo hivyo Wakristo wanavyokumbuka jinsi

nguvu za Yesu zinavyowatoa watu wake katika utumwa wa dhambi.

Wakati mtumwa anapomkumbuka Yesu Kristo, ni lazima akumbuke jinsi alivyokombolewa. Divai na mkate havina maana ye yote kwa waamini. Bali hupata maana yake kutoka kwa yule ambaye vitu hivi vina-mkumbusha. Ina maana gani kumkumbuka Yesu? Kumkumbuka Yesu ni kukiri kwamba ni Mwokozi anayetawala ambaye anaishi.

Je! ni matakwa gani ambayo Paulo alitoa katika kifungu cha 28 yahusuyo wale wanaotaka kula Chakula cha Bwana? Mtu anapojitayarisha kula chakula cha Bwana, anapaswa ajihoji mwenyewe ili aone mahitaji na makosa yake. Kila Mkristo ana dhambi maishani mwake. Hakuna ye yote ambaye ni Mkamilifu. Lakini kila Mkristo anapaswa kukua na kumwacha Roho Mtakatifu amfanye awe kama Yesu. Mkristo anapaswa kumwomba Mungu amsamehe dhambi zake kila mara. Yeye tu ndiye awezaye kutufanya tufae kukaa mezani pake. Kila Mkristo anapaswa kuja akiwa anatubu dhambi zake na kumwomba Mungu amfanye afae kule ba'ala ya kukaa mbali.

Paulo anasema wazi katika kifungu cha 27 kwamba ikiwa mtu atashiriki katika Chakula cha Bwana na roho usiyostahili, huwa anaharibu maana ya agizo hili. Kila Mkristo anapaswa kuja na roho wa kutubu na kwa unyenyekevu. Anapaswa kuwazia hasa kwa kukumbuka yale ambayo Bwana Yesu Kristo amefanya maishani mwake. Anapaswa kusikia mwito wa

kujitoa kabisa kwa kumtumikia Mungu. Iwapo atakuja na roho kama hii, basi hapaswi kuwa na wasiwasi juu ya kushiriki katika Chakula cha Bwana kwa njia isiyostahili.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuelewa maana ya kweli ya Chakula cha Bwana ili waweze kukishiriki kwa njia ifaayo.

KULIFUNDISHA SOMO

Chukua na uinue juu ile karatasi ambayo umeandika maana ya neno agizo. Utapaswa kuandika usemi huu ubaoni iwapo hakuna karatasi au haujaandika po pote. (Agizo ni sharti au amri ya Yesu ambayo ingali inafuata na kanisa.) Jadiliana juu ya usemi huu.

Uliza: Je! tulijifunza juu ya agizo lipi wiki iliyopita? (Ubatizo)

Sema: Makanisa mengi ya Kibatisti hufuata hasa maagizo mawili tu, ubatizo na Chakula cha Bwana.

Uliza: Je! ni nani anayepaswa kushiriki katika Chakula cha Bwana? (Wale ambao wamempokea Yesu Kristo kama Bwana na kubatizwa.)

Gundua yale Biblia isemayo. Sema: Leo tunataka tujifunze Maandiko kutoka sehemu mbili za Biblia ili tuelewe vyema maana ya Chakula cha Bwana. (Soma au uwaambie wanafunzi wawili wasome Mathayo 26:17-19 na 26-28.)

Tumia maelezo yaliyoko katika kitabu cha mwanafunzi na cha mwalimu kwa kuzungumza juu ya vifungu hivi. Usiwasimulie tu maelezo

yote. Uliza maswali ili wanafunzi hao waweze kupata maelezo haya wao wenyewe. Hakikisha kwamba umezungumzia pamoja mawazo yafuatayo:

-Mahali ambapo jambo hili lilifanyiwa (wakati wa sikukuu ya Pasaka kabla ya kusuliwa kwa Yesu).

-Maana ya Pasaka kulingana na historia ya Waebrania.

-Uhusiano kati ya Pasaka na Chakula cha Bwana.

-Maana ya vitu vinavyotumiwa, mkate na divai.

-Maana ya "agano" la Yesu jinsi lilivyotumiwa katika kifungu cha 28.

Sasa soma 1 Wakorintho 11:23-29. Sema: Paulo hakufurahishwa na jinsi kanisa la Korintho lilivyokuwa likishiriki katika Chakula cha Bwana. Inaonekana kama kwamba hawakuwa wametilia maanani, maana ya kweli ya agizo hili. Walikuwa wakitumia wakati huu kwa kufurahi na kuweza kula pamoja. Walikuwa wakiwakataza watu wengine isipokuwa wale waliokuwa katika kundi lao. Pengine matajiri walikuwa wakila chakula chote kabla maskini hawajafika. Baadhi yao walikunywa hata wakalewa sana. Hii haikuwa njia ambayo Chakula cha Bwana kilipaswa kuliwa, kwa hivyo Paulo alikuwa akijaribu kuwasaidia Wakorintho ili warekebishe makosa haya.

Jadili vifungu hivi. Tilia mkazo mawazo yafuatayo:

-Chakula cha Bwana huweza kutukumbusha yale ambayo Yesu ametufanyia.

-Wakati wa Chakula cha Bwana ni wakati wa kujichunguza sisi wenyewe.

-Huu ni wakati wa kuwa na ushirika na Mungu pamoja na Wakristo wengine.

Sasa zungumza juu ya kile ambacho Paulo alimaanisha alipowaonya Wakorintho kutoshiriki katika Chakula cha Bwana kwa njia isiyostahili. (Tazama mazungumzo ya kifungu cha 27 na 28 katika sehemu "Kujitayarisha Kufundisha.")

Eleza ukweli wa Maandiko haya katika maisha ya wanafunzi. Chunguza ni wanafunzi wangapi ambao ni Wakristo ambao wanashiriki katika Chakula cha Bwana. Iwapo kuna wale ambao hawashiriki, jaribu kutafuta sababu yake.

Sema: Yesu aliliambia kanisa lake kushiriki pamoja wakati huu ili kumkumbuka. Iwapo unakosa kufanya hivyo, basi wewe hujatii. Kumbuka pia huwa unakosa baraka maalum za wakati wa kushiriki na Kristo pamoja na washiriki wengine wa kanisa.

Zungumzia jinsi Wakristo wanapaswa kutenda wakati huu wa ibada maalum. Jaribu kuzungumza juu ya matatizo yo yote ambayo kanisa lako linalo kuhusu Chakula cha Bwana.

Wape wanafunzi wako muda wa kukamilisha sehemu yao ya "kazi ya kufanya". Sahihisha na kuzungumza juu ya majibu hayo.

KAZI YA KUḤANYA

Chora mstari kutoka kwa usemi wa kwanza uhusuo Chakula cha Bwana hadi kwa usemi wa pili ili ukamilishe sentensi zifuatazo.

sherehe.

Chakula cha wakati wa kuzungumza Bwana ni _____ na marafiki

wakati wa kukumbuka yale ambayo Yesu ametufanyia alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Mkate ni _____ mwili wa Yesu.
mfano wa _____

kwamba kila mmoja anapaswa kula mkate wakati wa sherehe.

kuwa na njaa.

Divai ni _____ damu ambayo Yesu alimwaga kwa ajili ya dhambi- zetu.
mfano wa _____

maji ambayo hayawezi kutuokoa.

Jibu maswali yafuatayo:

1. Je! makanisa mengi ya Kibatisti hutilia maanani maagizo mangapi? 2
2. Je! maagizo haya ni yapi? Ubatizo na Chakula cha Bwana.
3. Je! Yesu alishiriki Chakula cha Bwana kwanza na akina nani? wanafunzi wake.

4. Je! ni nani ambaye tunapaswa kumkumbuka wakati tunapokula Chakula cha Bwana? Yesu Kristo.
5. Je! unadhani ni nini ambacho mtu anapaswa kukumbuka kuhusu Yesu wakati anapokula Chakula cha Bwana?

(Jibu la mwanafunzi)

Kamilisha kifungu hiki cha Biblia:

“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.” (1 Wakorintho 11:26)

Chora mviringo kwa vitu vile ambavyo vinahitajika kwa ajili ya Chakula cha Bwana.

mkate, divai, mahindi, tofaa, Wakristo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo” (1 Wakorintho 11:26).

Weka mezani au sakafuni fumbo la kifungu cha kukumbuka ambalo umelitayarisha. Waambie wanafunzi kwamba unataka uone jinsi wawezavyo kuweka kwa haraka vijikaratasi hivi pamoja. Mmoja wao atapaswa kukisoma mara tu wamalizapo kukiunganisha pamoja. (Pengine utataka kutengeneza mafumbo aina mbili. Sasa utapaswa kuligawa darasa katika makundi mawili na kuwe na mashindano ya

kuona ni kundi lipi ambalo litamaliza kwanza.)

Jadili jinsi kanisa lako linavyoshiriki mara kwa mara katika Chakula cha Bwana. Jadili jinsi ulaji wa Chakula cha Bwana umetengewa tu washiriki wa kanisa. Wasaidie kuelewa kwamba ushirika wa kanisa huja baada ya kuokolewa. Mtu anaweza kuanza kufuata agizo la Yesu la

kumkumbuka kwa kula Chakula cha Bwana baada ya kumpokea kama Bwana na Mwokozi wake.

WAKATI WA MWISHO

Funga kwa maombi ya kwamba tutaweza kufahamu jinsi ya kushiriki katika Chakula cha Bwana, kwa njia ambayo itampendeza Mwokozi wetu.

SURA YA SABA

VIONGOZI WA KANISA

MASOMO YA BIBLIA: 1

Wakorintho 12:4-11; Matendo 6:1-6

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Pengine wengi wao ni washiriki wa kanisa. Au pengine wanataka kujua jinsi wawezavyo kusaidia katika kazi ya kanisa. Wajibu wao wa kwanza ni kujifunza yale ambayo viongozi wanafanya na aina ya watu ambao wanapaswa kuwa. Watatumia muda mwingi katika somo hili kujifunza juu ya kazi ya viongozi wa kanisa. Watagundua jinsi kanisa la mwanzo lilivyowachagua baadhi ya viongozi wake.

Wasaidie wanafunzi hao waelewe kwamba kuna kile ambacho wanaweza kufanya hata ingawa hawajakuwa wakubwa wa kuweza kufundisha Shule ya Jumapili au waongoze nyimbo. Somo la 1 Wakorintho 12:4-11 lapaswa kuwasaidia kuelewa kwamba Mungu amempa kila Mkristo karama fulani. Karama hizi zinapaswa kutumiwa kwa kumtumikia Mungu na kulijenga kanisa.

Tayarisha karatasi kubwa (orodha) ambayo utatumia kwa kufundisha juu ya viongozi wa kanisa. Andika maneno yafuatayo katika upande wa juu au wa kushoto wa karatasi hilo: MCHUNGAJI, SHEMASI, MWALIMU WA SHULE YA JUMAPILI, KIONGOZI WA NYIMBO. Acha nafasi ya kutosha

chini ya kila kichwa ili uandike yale ambayo kila kiongozi hufanya.

Pengine utataka kumwalika mmojawapo wa kiongozi wa kanisa lenu kuja na kuzungumzia kwa ufupi juu ya kazi yake.

Soma 1 Wakorintho 12:4-7. Paulo amezungumza sana hasa juu ya umoja wa kanisa katika barua hii kwa Wakorintho. Hata hivyo, kuwa na umoja haimaanishi kuwa ni lazima wote wafanane, wafikirie kitu kimoja au wote waweze kufanya jambo lile moja. Mkazo uliopo hapa ni kwamba kuna kazi tofauti kanisani ambazo zapaswa kufanywa, nao washiriki wana karama tofauti za kuwawezesha kutekeleza kazi hizi. Jambo muhimu la kukumbuka ni kamba kila karama hutolewa na Rdho yule yule. Hakuna karama ambayo imekusudiwa kutumiwa kwa ajili ya sifa au utukufu wa mtu aliyonayo, bali kwa manufaa ya kanisa lote.

Paulo anaorodhesha baadhi ya karama hizi. Hutapaswa kujifunza kwa ukamilifu juu ya karama hizi ili ujue somo hili. Ni muhimu kuwaambia wanafunzi wao kwamba karama ambazo Mungu amewapatia watu wake za kutumia mikono yao ni za muhimu sana kama kuwa na karama ya kufundisha au kuhubiri na kadhalika.

Matendo 6:1-6 inatupa funua jinsi kanisa la mwanzo lilivyofanya uamuzi na jinsi lilivyochagua viongozi wake.

Kanisa la Yerusalemu lilikuwa hasa na makundi mawili. Kundi la kwanza lilikuwa la Wayahudi wa Kipalestina. Ni Wayahudi ambao waliongea Kiebrania na ambao walitii desturi za Kiyahudi. Kundi lingine lilikuwa la Wayahudi wanaoongea Kiyunani. Wayahudi hawa hawakuwa wakiishi Palestina nao hawakufuata desturi zote za Kiyahudi. Wayahudi wa Kipalestina walijiona kuwa bora zaidi kuliko wale waliosema Kiyunani.

Wale washiriki waliosema Kiyunani waliona kama kwamba wajane wao hawakuwa wakitendewa mema katika "huduma ya kila siku." Huduma hii ingekuwa ya chakula, pesa au haya yote. Kulingana na Biblia wajane ndio waliokuwa maskini sana kwa kila kundi.

Mitume waliitisha mkutano wa kanisa ili kutaka kusuluhisha manung'uniko haya. Wao walijisikia kama Mungu alikuwa amewaita ili wajitoe kwa ajili ya maombi na kuhubiri. Kwa hivyo, waliwaambia washiriki wa kanisa wachague wasaidizi ambao walihitajika. Wasaidizi hawa walipaswa wawe watu ambao ni waaminifu na ambao wanaheshimika. Walipaswa kuwa na hekima ya kuweza kusuluhisha matatizo ambayo yangukwepo. Walipaswa pia wajitoe kwa kazi hiyo na wamtii Mungu.

Watu wote waliochaguliwa walikuwa na majina ya Kiyunani. Wanafunzi wengi waliosoma Biblia wanafikiria kwamba hii ilionyesha hitaji la kanisa la kutaka kuwatendea wema kabisa Kiyunani.

Mitume waliwatenda watu hawa saba kwa ajili ya kazi hii. Kuwekewa mikono kulikuwa njia ya kuonyesha kwamba washiriki fulani wanatengwa kwa ajili ya kazi fulani maalum.

Watu hawa saba huwa wanatajwa kama mashemasi wa kwanza. Biblia haitumii jina hili wakati inapoelezea juu yao, lakini mashemasi wa makanisa ya siku hizi huwatazama watu wale saba kama mfano wa wasaidizi wa kanisa.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi waelewe kazi na sifa za viongozi wa kanisa ili waanze kufikiria jinsi wawezavyo kufanya kazi kanisani kwa kutumia karama za Roho walizonazo.

KULIFUNDISHA SOMO

Mchague mwanafunzi mmoja awe anayehoji au "msimulizi". Waache wanafunzi wajitoe wenyewe kusoma sehemu ya mchungaji, shemasi, mwalimu wa Shule ya Jumapili na kiongozi wa nyimbo. Waache wasome sehemu zilizoko katika kitabu cha mwanafunzi. Mwache mwanafunzi mmoja aorodheshe yale uliyotayarisha yahusu kazi ya mchungaji, baada ya mchungaji huyo kuhojiwa. Jadiliana kuhusu kazi ya mchungaji. Fuata mtindo huo huo kwa kuzungumza juu ya shemasi, mwalimu wa Shule ya Jumapili na kiongozi wa nyimbo. Usitumie muda mwingi kwa kujadiliana juu ya watu hawa. Utapaswa kuwa na wakati wa kutosha kwa kuzungumza juu ya Maandiko ya vifungu.

Gundua yale Biblia isemayo. Mwambie msomaji mzuri asome 1 Wakorintho 12:4-11. Vifungu hivi havitakuwa rahisi kwa wanafunzi kuvielewa. Kwa hivyo tumia maelezo yaliyoko katika sehemu ya "Kujitayarisha Kufundisha" ili ueleze yafuatayo:

-Paulo alitilia mkazo hitaji la umoja katika kanisa.

-Mungu amewapa washiriki wa kanisa karama tofauti kupitia kwa Roho wake.

-Mkristo anapaswa kutumia karama zake kwa kumtukuza Mungu na kulijenga kanisa.

Uliza: Je! umewahi kuifikiria karama ambayo Mungu amekupatia? (Waache wanafunzi wajiadiliane juu ya yale wanayodhania kwamba wanaweza kufanya kanisani.)

Uliza: Je! kufundisha ni muhimu sana kuliko kuimba katika kwaya? (Jadili juu ya ukweli kwamba jambo muhimu hasa ni kutumia karama ambayo Mungu amekupa ili umtumikie. Mtu ye yote hapaswi kujivuna kwa sababu amepewa madaraka ya kuwa kiongozi katika kanisa.)

Waambie sasa wanafunzi wasome kifungu kimoja kimoja katika Matendo 6:1-6.

Uliza: Je! kunaye awezaye kusema tatizo lililokuwa katika kanisa la Yerusalemu? (Utapaswa kueleza jinsi hali ilivyokuwa kati ya Wayahudi wa Kiyunani na Wayahudi wa Kipalestina iwapo hakutakuwa na ye yote ambaye atataka kueleza.)

Uliza: Je! mitume na washiriki wa kanisa walisuluhishaje tatizo hili? (Waliwachagua watu saba ambao walikuwa washiriki wa kanisa ili wawasaidie wajane hao.)

Jadili jinsi mtindo huu unavyo-elekeana na ule unaofanywa na makanisa yetu ya kisasa kwa kuwachagua mashemasi. Jadili jinsi wanavyotengwa kwa ajili ya kazi hii.

Ikiwa ulimwalika shemasi kuja darasani mwako, sasa ndio wakati wa kumwambia awaeleze wanafunzi kwa ufupi kazi ambayo shemasi hufanya.

Wasaidie wanafunzi kukamilisha sehemu ya "Kazi ya Kufanya." Hakikisha kwamba majibu yao ni sahihi. Jadili juu ya majibu yao.

KAZI YA KUFANYA

Chora mstari kutoka kwa jina la kiongozi wa kanisa hadi kwa usemi ambao unaeleza kazi ambayo yeye hufanya.

Mchungaji	hufundisha Biblia kila Jumapili.
Shemasi	huongoza nyimbo wakati wa ibada.
Mwalimu wa Shule ya Jumapili	huhubiri na kutembelea.
Kiongozi wa Nyimbo	humsaidia mchungaji katika kutembelea na kutayarisha Chakula cha Bwana.

Kamilisha kifungu kifuatacho cha Biblia:

“Basi pana tofauti za karama; bali ni Roho yeye yule.” (1 Wakorintho 12:4)

Weka alama (✓) kando ya sentensi za kweli.

- ✓ Ni lazima viongozi wamwombe Mungu na wamwulize msaada.
- Ni lazima viongozi wawe na umri upatao miaka hamsini.
- Viongozi hawapaswi kwenda kanisani mara kwa mara.
- Ni lazima viongozi wawe na elimu.
- ✓ Ni lazima viongozi watumike kwa sababu wanampenda Mungu, bali sio kwa sababu majivuno.

Pangua herufi zifuatazo ili upate maneno yanayoeleza yule anayetoa karama na vipawa vyote. (1 Wakorintho 12:11)

HORO TAMKAFUTI

ROHO MTAKATIFU

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote” (1 Wakorintho 12:6).

Jifunzeni kusema kifungu cha kukumbuka. Sasa mwulize mmoja aeleze yale anayofikiria ndiyo maana yake.

Zungumzia jinsi Mungu anavyotumia Roho wake kumpa kila Mkristo karama. Hatupaswi kufikiria kwamba karama moja ni bora zaidi kuliko nyingine. Wala hatupaswi kujivunia karama hiyo.

Waambie wanafunzi ambao ni washiriki wa kanisa kufikiria juu kazi moja wawezayo kufanya ili watumike kanisani. Waambie waandike kazi hiyo katika ukurasa wa mwisho wa somo hili.

WAKATI WA MWISHO

Ongoza katika maombi ya kwamba wanafunzi watatumia karama waliyopewa na Mungu kwa kulijenga kanisa na kumtukiza Mungu.

MSHUHUDIE KRISTO -- NYUMBANI

MASOMO YA BIBLIA: Marko 5:1-20

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wanaelewa neno hili "kushuhudia?" Mkristo anayeshuhudia ni yule ambaye anawaambia wenzake yale ambayo Kristo amemfanyia. Si lazima mtu huyo aende katika sehemu nyingine ya pale anapoishi, au katika nchi nyingine ili awaambie watu habari za Mungu. Kila mmoja anaweza kumshuhudia Kristo pale anapoishi na kule aendako shuleni au anakofanya kazi.

Jaribu kutafuta picha mbili kutoka kwa gazeti. Picha moja itapaswa iwe ya kijiji au mji wa nchi yako. Ie nyingine itapaswa iwe ya nchi ya mbali ambayo ina watu tofauti na wanaovaa tofauti. Shikamanisha picha hizo kwenye karatasi au ubaoni. Andika maneno haya juu ya picha hizo: JE! NITASHUHUDIA WAPI?

Somo hili litawasaidia wanafunzi wako kujua umuhimu wa kuwa shahidi wa Kristo. Mwombe Mungu aweze kukusaidia ili ufundishe somo hili kwa njia ambayo itawafanya wanafunzi hao waamue kuanza kumshuhudia Yesu wiki hii.

Watu wa Mataifa walikuwa wakiishi katika nchi ya Gerasi. Nao Wayahudi hawakuwa wakifuga nguruwe.

MTU MWENYE PEPO WACHAFU
Soma Marko 5:1-5

Yesu na wanafunzi wake walikutana na mtu mwenye pepo wachafu

waliposhuka kutoka katika mashua yao walipoifikia nchi ya Gerasi. Mtu huyu aliishi karibu na ziwa katika kilima ambapo palizikwa wale wafu. Mtu huyu mgonjwa alikuwa mwenye nguvu nyingi, na hapakuwa na mtu ye yote ambaye angeweza kumfunga hata kwa minyororo. Alikuwa akipiga kelele usiku na mchana na alikuwa akijikatakata kwa mawe.

Wakati mtu huyu wa pepo wachafu alipomwona Yesu, alimkimbiliana na akapiga magoti mbele yake. Pepo wale walimfanya aulize hivi, "Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese." (Marko 5:7) Pepo hao alimfahamu Yesu kwa sababu walimwita kwa jina lake. Walijua kwamba Yesu alikuwa na uwezo mkuu kuwashinda nao hawakutaka wasumbuliwe.

Jina la Mtu Huyo Mgonjwa (Soma Marko 5:6-10).

Yesu aliwaamuru pepo hao wachafu wamtoke mtu yule. Halafu Yesu akamwuliza jina lake. Naye akamwambia anaitwa "Legioni" lenye maana ya "wengi". "Legioni" ilikuwa sehemu moja ya jeshi la Kirumi ambalo lilikuwa na wanajeshi wapatao elfu sita. Kwa hivyo tunajua mambo matatu juu ya pepo hawa wachafu kutokana na jina lake: (1) walikuwa wengi (2) walikuwa wamejiandaa kutenda maovu na (3) walikuwa na nguvu nyingi.

Yesu Anamponya Mtu Mwenye Pepo Wachafu (Soma Marko 5:11-13).

Yesu alimponya mtu huyu kwa kuwakubalia pepo wale kuingia ndani ya nguruwe. Nguruwe hawa walisumbuliwa sana na pepo wale walipowaingia. Jambo hili liliwafanya nguruwe wapatao elfu mbili kutelemka kwa kasi na kuingia baharini na mwishowe kufa humo.

Habari ya Uponyaji (Soma Marko 5:14-17).

Habari za mwujiza huu wa uponyaji zilisimuliwa kwote nchini hata mijini. Hatimaye watu hao walienda pale makaburini ili kujionea wenyewe mahali alipoishi mgonjwa yule. Watu hawa waliitikia kwa njia ya ajabu sana. Walimwambia Yesu aondoke nchini kwao. Hasa walihusika sana na jinsi walivyopoteza mali yao kuliko walivyomfikiria mtu yule alieponywa.

Itiko la Mtu Yule Aliyeponywa (Soma Marko 5:18-20).

Mtu yule aliekuwa ameponywa alitaka kwenda pamoja na Yesu, lakini Yesu alikataa. Akamwambia, "Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana."

Mtu huyu alimtii Yesu. Alienda mahali paitwapo "Dekapoli" ambapo pana maanisha "kumi". Hii inamaanisha kwamba aliendea miji kumi ya eneo hilo na kuwaambia watu wa huko habari za Yesu ambaye alikuwa amemponya.

Ukweli wa Kufikiria:

1. Yule mtu alieponywa alimtukuza Kristo kwa kuwaambia wenzake

jinsi Yesu alivyobadili maisha yake.

2. Watu waliosikia ushuhuda wake walitambua uwezo wa kuponya.
3. Imani ya mtu yule iliimarishwa alipozidi kuwaambia yale yaliyomkata.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwatia moyo wanafunzi ambao ni Wakristo kuweza kushiriki na jamaa zao na marafiki yale ambayo Kristo amewafanyia.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! umewahi kumwona mtu mwenye ugonjwa mbaya zaidi kama ukoma? (Ngojia majibu.)

Uliza: Je! unadhani ungejisikiaje ikiwa ulikuwa na ugonjwa mbaya kama huu? (Sikiliza majibu yao.)
Uliza: Je! unafikiri jamaa na marafiki zako watafurahia iwapo utaponywa ugonjwa mbaya kama huu?

Sema: Tutajifunza leo habari za mtu ambaye alikuwa na pepo wachafu. Alikuwa mgonjwa sana hata jamaa yake haingeweza kumsaidia. Siku moja, Yesu na wanafunzi walienda mahali ambapo mtu huyu alikuwa anaishi. Yesu alimponya na maisha yake yote yakabadilika. (Endelea kusimulia hadithi hii jinsi ilivyoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi.)

Uliza: Je! mnafikiri jamaa na marafiki wa mtu huyu walidhaniaye walipomwona? (Walishangaa sana. Walitaka kujua hasa jinsi alivyo-ponywa.)

Uliza: Je! unaweza kumwelezaje mtu huyu baada ya kuponywa na Yesu? (Alitulia wala hakupiga makelele. Haikumbidi kufungwa na minyororo ili asijikatakate wala kuwadhuru watu wengine. Alivalishwa nguo nzuri na hakuwa na akili ya uenda wazimu.)

Uliza: Je! watu walioishi katika eneo hili waliitikiaje? (Hawakufurahi na walimtaka Yesu aondoke.)

Sema: Yesu alifanya yale yaliyokuwa mema hata ingawa watu hawakumpenda. Tunaweza kutotendewa mema tunapowaambia wenzetu habari za Yesu. Watu hao wanaweza kutuchekelea au kutudhihaki. Lakini tunapaswa kuwa waaminifu jinsi Yesu alivyokuwa.

Uliza: Je! kwa nini Yesu alikataza mtu yule kwenda pamoja naye na wanafunzi wake? (Yesu alimtaka arudi nyumbani kwao na awashuhudie jamaa yake pamoja na marafiki.)

Uliza: Je! ushuhuda wa mtu yule ungekuwa wa muhimu ikiwa angeenda mahali ambapo watu hawakumfahamu? (La. Jamaa na marafiki zake walijua hali yake kabla ya kuponywa. Na sasa waliona mabadiliko ambayo Kristo alikuwa amefanya maishani mwake.)

Sema: Yesu anatutaka tuwe mashahidi wake sasa. Tunayo yale ambayo twaweza kusema tuliyoyapitia maishani mwetu. Hakuna ye yote awezaye kusema yale yaliyotupata.

Uliza: Je! Yesu anatutaka twende kumshuhudia wapi? (Waonyeshe zile picha iwapo unazo darasani.) Je!

anatutaka twende kumshuhudia katika nchi ya mbali? Au, anatutaka tuwaambie watu wa eneo letu, nyumbani, shuleni, na vijijini juu ya habari zake?

Sema: Si kila Mkristo ambaye anaweza kwenda katika sehemu nyingine au nchi ya kigeni na kuwaambia watu wa huko habari za Yesu. Lakini kila Mkristo anaweza kuwa shahidi mzuri pale anapoishi.

Uliza: Je! utashuhudia wapi wiki ijayo? (Wape muda wa kutaja pale ambapo watashuhudia.)

KAZI YA KUFANYA

Soma Marko 5:9. Andika vizuri herufi zifuatazo ili upate jina la mtu yule mwenye pepo wachafu.

GIELINO LEGIONI

Jaza nafasi iliyoachwa na jibu lililo sahihi:

1. "Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye Pepo mchafu." (Marko 5:2)
2. Mara kwa mara mtu yule alikuwa akifungwa kwa pingu na minyororo. (Marko 5:4)
3. Je! mtu yule mwenye pepo wachafu alijkatakata akitumia nini? Mawe (Marko 5:5)
4. Je! mtu yule alifanyaje alipomwona Yesu? (Marko 5:6) Alimkimbilia mbio na akam-sujudia.
5. Je! pepo wale wachafu walienda wapi baada ya Yesu kuwakemea

kutoka katika mtu yule? (Marko 5:13) Waliingia katika nguruwe.

6. Je! ni nguruwe wangapi waliokufa baharini? Walikuwa nguruwe wapatao elfu mbili

Weka alama (✓) kando ya sentensi ya kweli na upige mstari katika sentensi ambayo si ya kweli.

~~— Mkristo anaweza kushuhudia tu katika nchi ya mbali.~~

✓ Yesu alimwambia mtu yule mwenye pepo wachafu kurudi nyumbani kwao na waambie rafiki zake yale ambayo Yesu alikuwa amemfanyia.

✓ Mkristo anapaswa kuiambia jamaa na marafiki zake habari za Kristo.

Kamilisha hadithi ifuatayo kwa kutumia maneno yako mwenyewe.

Samweli alimkiri Yesu wakati wa mkutano wa ufufuo uliofanywa katika kijiji chake. Baadhi ya marafiki zake walianza kumchokoza aliporudi shuleni. Walimchekelea huku wakimwambia, "Tulisikia kwamba ulimpokea Kristo wiki iliyopita. Ukristo haufai vijana hodari kama sisi. Unafaa tu wanawake na wasichana." Samweli akawaambia, " (Jibu la mwanafunzi)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"...Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu" (Marko 5:19)

Uliza:

1. Je! Yesu alimwambia mtu huyu aliyeponywa kwenda wapi? (Nyumbani kwake)
2. Je! alitakiwa awashuhudie akina nani? (Marafiki zake)
3. Je! alitakiwa awaambie nini? (Yale ambayo Bwana alikuwa amemfanyia)

WAKATI WA MWISHO

Waambie wanafunzi hao wafunge macho yao na wamfikirie mtu mmoja ambaye wanajua kwamba anapaswa kumjua Yesu. Sasa waambie wamwombe mtu huyu kimoyomoyo.

Omba ukimwuliza Roho Mtakatifu awasaidie wanafunzi hawa waweze kumwambia mtu mmoja habari za Yesu wiki ijayo.

MSHUHUDIE KRISTO -- KWA MAJIRANI

MASOMO YA BIBLIA: Maiendo
10:24-39

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wanashirikiana vizuri na watu wa kabila lingine, rangi au dini? Au, Je! wanawaepa watu ambao hawaongei lugha moja nao au wenye desturi tofauti na zao?

Somo letu la leo litawajulisha hitaji la kuwashuhudia jirani zao. Jirani zao wanaweza kuwa watu ambao wanatoka eneo moja nao. Au, wanaweza kuwa wanatoka katika nchi jirani, au wawe watu wa rangi nyingine.

Waombee washiriki wa darasa lako. Wataweza kujifunza wiki hii ukweli wa kiroho ambao utabadili nia zao katika maisha yao yote.

Soma kwa makini maandiko ya somo hili. Hutawaambia wanafunzi hawa kila kitu ambacho utajifunza katika somo lako. Hata hivyo uelewaji wako utakusaidia kuweza kulifanya somo hili kuwa la muhimu kwao.

Wafikirie watu wa jamii na kanisa lako ambao ni wa makabila mbali mbali, wanatoka sehemu tofauti, au nchi nyingine. Uwe tayari pamoja na wanafunzi wako kutafuta njia ambazo wanaweza kuzitumia kwa kuwasaidia watu wengine na kuwashuhudia juu ya habari za Kristo.

Somo letu la wiki iliyopita lilitukumbusha kwamba tunapaswa

kumshuhudia Kristo nyumbani kwetu. Hapa ndipo mahali pazuri pa kuanzia. Hata hivyo ushuhuda wetu hauishii hapo. Tunao wajibu wa kumshirikisha Kristo kwa watu wale ambao hawatujuu. Watu wa makabila mengine, nchi na imani tofauti za kidini wanapaswa kumjua Kristo.

Kulingana na maandiko ya somo la leo, tunajifunza jinsi mtume Petro alivyowashuhudia Watu wa Mataifa. Petro alikuwa Myahudi. Alionekana, akatenda na akaongea kama Myahudi. Hali na fikira zake zilimfanya ajisikie kwamba Wayahudi walikuwa bora zaidi kuliko Watu wa Mataifa. Hata hivyo, Mungu alikuwa amewachagua Wayahudi kuwa watu ambao angewatumia kwa kuuleta wokovu kwa ulimwengu wote. Yesu, Mwokozi, alizaliwa katika nyumba ya Kiyahudi. Mungu alimfundisha Petro jambo muhimu. Mpango wake wa wokovu kwa Wayahudi, uliwahusu hata Watu wa Mataifa.

Utapaswa kusoma Matendo 10 ili uweze kuelewa vizuri maandiko ya somo la leo. Baadhi ya mambo muhimu ni:

1. Kornelio alikuwa akida wa jeshi la watu wa Mataifa ambaye aliheshimiwa sana, naye aliishi pale Kaisaria. Alikuwa mcha Mungu na alihimiza jamaa yake kumcha Mungu.
2. Mungu alisema na Kornelio katika maono na akamwambia

amtume mtu pale Yafa ili kwenda kumwita Simoni Petro. Kornelio aliwatuma watu wawili kwenda kumtafuta Petro siku iliyofuata.

3. Wakati huo huo Mungu alinena na Petro katika maono. Aliona nguo kubwa kama shuka ikishuka kutoka mbinguni ambayo ilikuwa na aina yote ya wanyama. Alisikia sauti ikimwambia aondoke na aende kuzila. Petro alihangaishwa sana. Yeye alikuwa Myahudi nao Wayahudi hawakukubaliwa kula wanyama ambao walifikiriwa kuwa ni "najisi". Sauti hiyo ilimjia mara tatu ikimwambia kwamba ale nyama zile.
4. Wakati huo huo, wale watu ambao walitumwa na Kornelio walifika katika lango la nyumbani kwa Petro. Roho alimwambia Petro kwenda pamoja na wale ambao walikuwa wakimtafuta.

Kufika kwa Petro katika Nyumba ya Kornelio. (Matendo 10:24-33)

Petro na baadhi ya ndugu Wakristo walienda Kaisaria siku iliyofuata. Wakati Petro aliingia nyumbani humo, Kornelio alipiga magoti na akamsujudia. Petro alimkataza. Akamwambia, "Simama, mimi nami ni mwanadamu."

Haikosi Kornelio alishangaa sana kumwona Petro nyumbani kwake kwa sababu Wayahudi hawakuweza kuwatembelea Watu wa Mataifa. Petro hangeweza kwenda nyumbani kwa Kornelio bila ya kuona maono yale.

Kornelio naye alimwelezea juu ya maono ambayo Mungu alikuwa amemwonyesha. Maono haya yalimfanya Kornelio awaalike watu wengi wakutanike kwake ili wamsikilize Petro akizungumzia habari za Mungu.

Mahubiri ya Petro (Soma Matendo 10:34-39)

Petro alianza ujumbe wake kwa kuwaambia kwamba neema ya Mungu ni kwa kila mmoja. Hili ndilo jambo ambalo Mungu alimfundisha, na sasa alikuwa akiwaelezea Watu wa Mataifa.

Hatuwezi kufikia matokeo ambayo maneno haya yalitoa kwa wale waliomsikiliza Petro. Hawakuwa wamewahi kukubaliwa kuingia hekaluni. Hapakuwa na makuhani wa kutoka kwa watu wa Mataifa. Na sasa walikuwa wakiambiwa kwamba Mungu hapendelei kabila moja kuliko lingine.

Ni lazima ujumbe wa Petro uwe ule ambao tunatoa sasa. Hakuna kabila au taifa ambalo ni bora zaidi kuliko lingine mbele za Mungu. Nia na matendo yetu kwa wenzetu hudhihirisha wazi yale tuliyojifunza kutoka kwa somo hili ambalo Mungu alimfundisha Petro.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuweza kupanga jinsi watakuwa mashahidi wa Kristo kupitia kwa matendo yao na yale wasemayo.

KULIFUNDISHA SOMO

Wafanye wanafunzi wakusikilize kwa kuwaambia hadithi ifuatayo:

Yohana na Benson walikuwa vijana Wakristo. Wote walihudhuria kanisa kwa uaminifu. Walikubaliana kwamba iliwapasa washiriki wa kanisa wawashuhudie watu wengine habari za Kristo. Walipaswa pia kuwasaidia watu wa jamii yao.

Siku moja mwalimu wa Shule ya Jumapili aliliambia darasa hilo habari za jirani ambaye alikuwa mgonjwa. Mtu huyu alikuwa ametoka katika nchi nyingine na hakuongea lugha moja nao. Alikuwa na shamba dogo na mifugo, lakini sasa hangeweza kuwatunza. Mwalimu yule alimtaka mtu ambaye angejitoe kwa siku chache ili awatunze mifugo wale wa mzee yule mgonjwa.

“La, hashu, siwezi kufanya hivyo,” Yohana akasema. “Kwa sasa nina kazi nyingi.”

“Ningefurahi sana kumsaidia yule jirani yetu mgonjwa.” Benson akasema “Nitaenda kwake kesho asubuhi na mapema ili asiye akawawazia mifugo hao wake. Niombeeni pia ili niweze kumwambia kwamba Mungu anampenda.”

Uliza: Je! ni kijana yupi ambaye alikuwa tayari kuwasaidia wenzake? (Benson)

Uliza: Je! Benson alionyesha je upendo wa Mungu? (Alionyesha kwa matendo.)

Sema: Mara kwa mara Wakristo wengi huongea juu ya upendo wa

Mungu kwa watu wote lakini huwa wanasema tu. Matendo yao wafanyayo hayaonyeshi kamwe upendo wa Mungu.

Uliza: Je! ni watu gani ambao tunapaswa kuwashuhudia juu ya upendo wa Mungu? (Watu wote kila mahali)

Uliza: Je! ni vizuri kuwaambia watu juu ya Yesu Kristo, au kuwaonyesha upendo wa Mungu kwa matendo na yale usemayo? (Yote mawili yanahitajika.)

Sema: Twajifunza katika somo letu la Biblia kwamba Mungu alimfundisha Petro kwamba upendo wake ulikuwa ni wa watu wote. Mungu alimdhahirishia wazi Petro katika maono kwamba watu wote, yaani Wayahudi na Watu wa Mataifa, ni sawa mbele za Mungu.

Simulia kwa ufupi hadithi ya maono ya Petro na safari yake ya kwenda kuhubiri nyumbani kwa Kornelio.

Uliza: Je, unafikiri kwamba kabila au lugha yako ni bora zaidi kuliko ya watu wengine ambao unawafahamu?

Sema: Wewe si shahidi mwema wa Yesu Kristo iwapo unawafanyia mzaha watu wengine au makabila mengine.

Waambie wanafunzi hao kutaja watu wa kijiji chao au kanisa ambao wanatoka katika nchi nyingine au wanaongea lugha tofauti na yao. Andika majina yao ubaoni.

Uliza: Je! tunaweza kutumia njia zipi kuwaonyesha kwamba tuna-


Uliza: Je! Yesu alisema tunapaswa kuwa mashahidi wapi? (Yerusalemu, Uyahudi, Samaria na mwisho wa nchi.)

Mwisho wa Nchi

Samaria

Uyahudi

Yerusalemu



Sema: Watu ambao si Wakristo wanatutazama sisi. Watasikiliza yale tusemayo iwapo tutawaonyesha kwanza kwa matendo yetu kuwa Mungu anawapenda.

Chora mstari kutoka mwanzo wa sentensi hadi ile sehemu iliyo ya kweli.

mtu ambaye anawa-
ambia wenzake habari
za upendo wa Mungu
kwa matendo au yale
asemayo.

Weka alama (✓) kando ya sentensi iliyo sahihi.

—Monika hakusikiliza yale ambayo aliambiwa na mchungaji wake.

✓ Monika alitaka kujua jinsi alivyotakiwa kuwashuhudia wenzake na kuwasaidia.

—Monika alitaka tu kuongea na mama yake ili asifanye kazi ya kusaga mahindi.

Chora mviringo kwenye mambo yale ambayo unaweza kufanya ili uwasaidie wale wasio Wakristo kujua kwamba unawapenda na pia Mungu anawapenda.

1. Nimsaidie mama mzee kubeba kuni.

2. Ni wachokoze watoto wa jirani na kuwafanya walie.

3. Nimsomee kipofu Biblia.

4. Nifiche kifaa cha mtoto cha kuchezea.

5. Nimpelekee mama mgonjwa chakula.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

Je! Yesu anatupa nani ambaye atatusaidia kushuhudia?

ROHO MTAKATIFU

Je! Yesu aliwaambia wanafunzi wake washuhudie wapi?

Katika Yerusalemu na katika Uyahudi wote na Samaria na hata mwisho wa nchi.

Yesu alikuwa Yerusalemu pamoja na wanafunzi wake alipowaamuru hivi. Kwa hivyo aliwataka waanze kushuhudia pale walipo. Andika jina la kijiji au mji wako katika nafasi ifuatayo. Hii ndiyo Yerusalemu yako.

Uyahudi ilikuwa ni pamoja na eneo lote ambalo lilitumia Yerusalemu kama mji mkuu. Andika baadhi ya majina na vijiji au miji ambao iko katika eneo lako au mkoa wako.

Yesu anawataka wafuasi wake kushuhudia pia katika sehemu hizi.

Samaria ilikuwa ni eneo ambalo lilikuwa mbali na lenye desturi tofauti na za Uyahudi. Hasa Watu wa Mataifa ndio walioishi Samaria nao Wayahudi hawakuwa marafiki na Wasamaria. Andika majina ya nchi ambazo ni jirani na nchi yako.

Watu wa huko wanaweza kuongea lugha tofauti. Pengine serikali ya nchi

yako haiwezi kuwa na urafiki na serikali ya nchi jirani. Lakini Mungu yungali anawataka wafuasi wake kuwa mashahidi wa nchi hizo pia.

Mwishowe Yesu alisema twende hadi mwisho wa nchi. Kila mtu amehusishwa katika amri hii. Anawataka watu wote wajue upendo wa Mungu na wokovu ambao anawapatia kupitia kwa kifo chake pale msalabani.

WAKATI WA MWISHO

Uliza: Je! utakuwa shahidi wa Kristo wiki hii kwa kumsaidia mtu wa taifa au kabila lingine? Utamwonyesha kwamba Mungu anampenda kwa yale unayotenda, wala sio tu kwa yale usemayo.

Waambie wanafunzi watatu waombe mambo yafuatayo.

-kwamba Mungu atasamehe ubaguzi wo wote uliyoko moyoni mwa mtu ye yote ambao utamzuia asiwe shahidi mwema.

-kwamba Mungu atamwonyesha kila mmoja yule ambaye atamshuhudia wiki hii.

-kwamba kila mmoja atakuwa na ujasiri wa kusema neno la upendo wa Mungu kwa yule ambaye hajaokoka.

SURA YA KUMI

MSHUHUDIE KRISTO -- ULIMWENGUNI

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo
28:18-20

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wanaelewa maana ya maneno haya, "Agizo Kuu?" Je! wanafahamu ni nani ambaye Kristo alimwagiza hivi na kwa nini alimwagiza hivyo?

Somo la leo litawasaidia wanafunzi wako kuelewa maana ya agizo hili la Kristo kwa wanafunzi wake na kwetu sisi pia. Watajifunza pia maana ya "Jumuiya ndogo ya Makanisa," na "Jumuiya Kuu." Wataelewa jinsi wawezavyo kuwa na sehemu ya kutimiza agizo hili la Kristo hata ingawa wangali shuleni (wanafunzi).

Jaribu kutafuta habari ifuatayo wakati wa wiki:

1. Jina la Jumuiya yako ya Kibatisti.
2. Idadi ya makanisa yaliyo washiriki wa jumuiya yako.
3. Jina la kiongozi wa jumuiya hiyo.
4. Jina la kiongozi wa jumuiya kuu.
5. Majina ya wamisheni ambao wanasaidiwa kupitia kwa jumuiya yako.
6. Jumla ya pesa ambazo kanisa lako lilitoa mwaka uliopita ili kusaidia jumuiya ndogo na jumuiya kuu.

Tafuta ramani ya nchi yako iwapo inaweza kupatikana. Onyesha kwenye ramani hiyo jumuiya mbalimbali,

halafu uweke alama za kuonyesha mahali ambapo wamisheni wanafanya kazi.

Omba kwamba Mungu atatumia somo hili kuwawezesha wanafunzi kutambua hitaji lao la kushiriki katika umisheni. Waombee wanafunzi ili wajitoe waweze kutumiwa na Mungu kama wamisheni, mchungaji au viongozi katika kanisa.

Soma Mathayo 28:18-20.

Yesu alijitokeza mara nyingi sana kwa wanafunzi kwa muda wa siku arobaini zilizofuata baada ya kufufuka kwake. Aliwapa wanafunzi wake kazi muhimu sana alipokuwa anajitayarisha kurudi mbinguni kwa baba yake. Aliwaambia wakawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wake.

Jukumu hili linaitwa Agizo Kuu. "Agizo" ni amri au sharti la kufanya kazi. Kazi hii ilipewa kwanza wanafunzi wake, lakini yatuhusu sisi pia. Wakristo wa kila kizazi wana wajibu wa kukiambia kizazi hicho habari za Yesu. Sisi ni Wakristo kwa sababu tuliambiwa habari za Kristo na mtu mwingine.

Mamlaka ya Yesu. Kulikuwa na wanafunzi kumi na mmoja wakati Yesu alipojitokeza kwao kwa mara ya mwisho. Wao walimshjudia. Naye Yesu alianza kuwaambia wanafunzi hao ujumbe wake muhimu kwa kuwaelezea juu ya mamlaka yake.

Yule ambaye alikuwa akiwaagiza alikuwa na mamlaka yote mbinguni na duniani. Hapakuwa na mamlaka mengine makuu.

Enendeni mkawafaye wanafunzi. Hili ndilo agizo la kwanza ambalo Yesu alitoa. Kazi hii inaweza kueleweka vyema kwa maneno haya, "Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi."

Mwanafunzi ni yule anayejifunza. Kuwa mwanafunzi kunamaanisha mtu ambaye anamfuata Mungu bila kujali gharama. Huduma ya Yesu ilihusu tu watu wa eneo lake. Sasa alitaka wanafunzi wake wachukue jukumu la kueneza mafundisho yake kwa mataifa yote.

Mkiwabatiza. Hili ndilo agizo la pili. Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kuwabatiza wale ambao walimpokea kama Mwokozi. Ubatizo haumwokoi mtu kutoka katika dhambi zake. Ni ishara ya kuonyesha kwamba mtu amemwamini Yesu kama Mwokozi wake.

Wale waliookoka walipaswa kubatizwa "kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu." "Jina" linasimamia yule mtu. Kubatizwa katika jina la Mungu kulimaanisha kubatizwa na kuwa mali ya Mungu.

Na kuwafundisha. Hili pia ni agizo la tatu. Waamini wapya wanapaswa kufundishwa. Lakini haimaanishi kwamba ni lazima kujua sana ili wamwelezee mwalimu. Tunapaswa kuwafundisha wanafunzi katika kutii yote ambayo Kristo ametuamuru. Mkazo wa jambo hili unahusu hasa utiifu, wala sio hekima.

Ahadi. "Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Yesu yu pamoja nasi sikuzote: tunapokuwa pweke, tuwapo na maumivu, tunapokata tamaa, tuwapo wenye furaha na hata wakati wa huzuni.

Wanafunzi wangepata ujasiri wa kuuendea ulimwengu wote kwa sababu ya kuwepo kwa Kristo. Walipokuwa na Kristo walikuwa wamepata cho chote walichohitaji.

Ahadi hii pia ni yetu. Tunapaswa kukumbushwa juu ya ukweli huu tunapowashuhudia wapotevu na kuona jinsi wanavyokataa. Hata hivyo, Yesu yu pamoja nasi.

Wajibu wa kanisa. Agizo Kuu linatuonyesha kwamba kusudi la Mungu lilikuwa la kufanya umisheni. Kusudi lake linapaswa kutimizwa kupitia kwa kanisa ili kuwasaidia watu kuweza kumwamini.

Umisheni huu ni pamoja na kushuhudia nyumbani na sehemu za mbali. Ulimwengu huu unahitaji Yesu. Sisi tunamjua na tuna wajibu wa kushiriki habari zake na wenzetu.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuelewa njia ambazo wanaweza kutumia kwa kutimiza Agizo Kuu.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Nataka wale ambao wamewahi kukimbia mbio za kupokezana vijiti wainue mikono yao. (Waitikie wale ambao wameinua mikono yao.)

Tunataka sasa tukimbie mbio za kupokezana vijiti hapa darasani. (Gawa darasa hili katika makundi mawili. Lipe kila kundi kalamu au kijiti kidogo. Mwambie mtu wa kwanza ampe yule aliyekaa karibu naye kalamu hiyo, hadi wote walioko katika kundi lake watapata kuishika kalamu hiyo.)

Mchezo huu utatusaidia kuelewa maana ya somo letu la leo.

Sema: Yesu alikuwa amekaa pamoja na wanafunzi wake kwa muda wa miaka mitatu. Sasa alikuwa akikutana nao kwa mara ya mwisho kabla ya kwenda mbinguni.

Alikuwa amefufuka siku arobaini zilizopita. Hata alikuwa amewatokezea wanafunzi wake mara nyingi baada ya kufufuka, lakini alikuwa yungali na mafundisho muhimu ambayo alitaka kuwaambia.

Uliza: Je! mnafikiri wanafunzi walijisikiaje wakati Yesu alipokuwa karibu kuwaacha? (Sikiliza majibu yao.)

Sema: Bila shaka walihuzunika sana kwa sababu hawangeweza kumwona uso kwa uso Mwokozi wao, lakini walifurahi pia, Kristo alikuwa amewaahidi kwamba watapokea Roho Mtakatifu wakati atakapowaacha. Hangeweza kuwa tu mahali pamoja. Angeweza kuwa na watu wote kwa wakati wote kupitia kwa Roho Mtakatifu - hata miaka elfu mbili baadaye.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Mathayo 28:18-20.

Uliza: Je! ni nani anayejua jinsi vifungu hivi vinavyoitwa? (Andika ubaoni neno Agizo Kuu.) Uliza: Je! maana ya "Agizo" ni nini? (Amri, kupewa kazi ya kufanya.)

Uliza: Je! ni nani waliopewa amri hii? (Wanafunzi)

Uliza: Je! kwa nini tunapaswa kufikiria juu ya jambo hili ikiwa ni wanafunzi tu waliomsikia Yesu akisema? (Hata nasi tunapaswa kulifanya.)

Sema: Tajeni mambo matatu ambayo yamo katika amri hii. (Enendeni, mkiwabatiza na kuwafundisha.)

(Eleza kila mojawapo ya maagizo haya ukitumia maelezo yaliyoko katika sehemu ya "Soma Mathayo 28:18-20.")

Uliza: Ninyi ni wanafunzi, lakini je, mnaweza kushiriki katika kutimiza maagizo haya ya Yesu? (Chora ubaoni picha ionyeshayo jinsi ya kushuhudia iliyoko katika kitabu cha mwanafunzi.)

Sema: Ndiyo, mnaweza kushiriki katika utimizaji wa Agizo Kuu hili sasa. Mnaweza kumshuhudia mpotevu (waonyeshe ubaoni). Au, unaweza kutoa pesa kupitia kwa kanisa ili zifanye kazi ya umisheni. Jambo hili humwezesha mtu kwenda na kushuhudia. Waweza pia kuwaombea wapotevu, na wale wanaohubiri na kuwafundisha.

(Zungumzia kwa ufupi juu ya jumuiya ndogo na jumuiya kuu na jinsi kanisa lako linavyoshiriki katika umisheni. Waonyeshe ule mfano

ulioko katika somo hili. Tumia muda wa kutosha kwa kujibu maswali yahasuyo jumuiya ndogo na jumuiya kuu yaliyoko katika somo la wanafunzi.)

Sema: Yesu alikamilisha kazi yake hapa duniani na angerudi mbinguni baada ya muda mfupi. Aliwapa wanafunzi wake wajibu wa kuendelea na kazi aliyoanzisha alipokutana nao kwa mara ya mwisho.

Uliza: Je! mchezo wetu wa mbio za kupokezana vijiti unatusaidiaje kuelewa sehemu yetu katika kazi ya Kristo? (Wakristo wa kila kizazi wanapewa wajibu wa kueneza ujumbe huu kwa kizazi chao.)

Sema: Kila mmoja wenu anasehemu yake. Ni lazima umshuhudie Kristo nyumbani kwenu, shuleni na hata kwa wale ambao wanatoka katika nchi zingine.

Sasa ni zamu yetu. Tunao wajibu mikononi mwetu.

Uliza: Je! Yesu aliwaahidiye wanafunzi wake? (Kwamba atakuwa pamoja nasi hata ukamilifu wa dahari.)

Sema: Yesu alituahidi uwepo wake pamoja nasi. Alitupatia pia nguvu za Roho Mtakatifu ambazo tungetumia kwa kufanya kazi hii.

Omba sasa ombi fupi la kumwuliza Mungu amsaidie kila mwanafunzi ili awe tayari kufanya cho chote ambacho Kristo anataka afanye.

KAZI YA KUFANYA

Andika hapo chini baadhi ya kazi ambazo zinaweza kufanywa na

waamini wa sasa kwa kutimiza Agizo Kuu la Kristo.

Kuwashuhudia wapotevu.

Kutoa sadaka za kuwatuma wamisheni.

Kuwaombea wapotevu.

Kuwapatia watu vifungu au Maandiko ya Biblia.

Kuwaonyesha wapotevu upendo.

Kufundisha na kuhubiria wengine neno la Mungu.

Piga mstari chini ya orodha ya maneno yafuatayo ambayo yanaeleza juu ya mwito wa Wakristo kwa ulimwengu.

mwenye kuomba

kushiriki

kuhusika

mwenye upendo

mpole

mwenye kumcha Mungu

msema ukweli

kutojali

mchoyo

mpweke

kufikiria nafsi yake

mkatili

kutopendelea

mtoaji

mwenye kuhurumia

mwenye kuhusika.

Chora mstari kutoka mwanzo wa sentensi hadi kwa sehemu ya pili ambayo itakamilisha vyema sentensi hiyo.

Makanisa ya nchi jumuiya ndogo.
moja huungana
pamoja ili kuunda

Mathayo 28:18-20 jumuiya kuu.
inajulikana kama

Kundi la makanisa Agizo kuu.
la sehemu fulani
huungana pamoja ili
kuunda

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Basi, Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari"
(Mathayo 28:18-20).

Ligawe darasa hilo katika makundi manne. Lipatie kila kundi sehemu moja ya kifungu cha kukumbuka. Liambie kila kundi liseme sehemu yake ukianza na wale walio na sehemu ya kwanza.

WAKATI WA MWISHO

Waambie wanafunzi hao wainamishie vichwa vyao na wafikirie kwamba Yesu anawapa kifimbo au kijiti cha kutumia katika mbio za kupokezana vijiti. Fikiria kuwa hii inaonyesha Injili ambayo wanatakiwa wawe na sehemu ya kuipeleka hadi kwa mataifa ya ulimwengu wote. Mwombe Mungu amwezeshe kila mmoja kuwa tayari kufanya mapenzi ya Mungu.

SURA YA KUMI NA MOJA UWAKILI WA MAISHA

MASOMO YA BIBLIA: 1

Wakorintho 6:19-20; 16:2; Malaki 3:10a

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wataweza kuelewa neno hili “wakili?” Wakili ni yule ambaye anasimamia mali ya mtu mwingine.

Somo hili linahusu kuwa mawakili wema wa vitu ambavyo Mungu ametupatia. Ametupa miili yetu, muda (wakati), vipawa, pesa na mali zingine. Hata hewa ambayo tunavuta, maua na miti ambayo tunafurahia, wingu na viumbe vingine vipo kwa ajili yetu. Kila kitu ni mali ya Mungu, lakini ametupa jukumu la kuvitunza na kuvitumia.

Waombee washiriki wote wa darasa lako. Mwombe Mungu akusaidie ili uweze kufundisha somo hili nao waweza kuutumia ukweli huu maishani mwao.

Watembelee washiriki wa darasa lako na uonyesha kuwa unapendezwa na maisha yao. Utaweza kufahamu iwapo wanatumia ukweli huu wanaojifunza iwapo utawatembelea.

Soma Malaki 3:10a. Nabii Malaki aliwalaumu Waisraeli kwa kumwibia Mungu zaka na sadaka. Amri ambazo walipewa na Mungu ziliwataka walete sadaka zao katika hazina ya Hekalu. (Mambo ya Walawi 27:30-34) Wao walikuwa hawafanyi hivyo. Mungu

sasa alikuwa anawataka watu wake watubu na walete zaka kamili katika nyumba yake ya kuabudia.

Mungu habadili nia yake. Watu wake wangali wanatakiwa kumrudia kwa kutoa sehemu ya kumi au zaka ya mali walizo nazo.

Mungu anatuahidi baraka kuu iwapo watu wake watakuwa waaminifu kwa kumtolea zaka. Sisi hukosa baraka hizi iwapo hatuchukui mafundisho haya kuwa ya muhimu.

Soma 1 Wakorintho 16:2. Paulo ametumia kifungu hiki kulishauri kanisa jinsi ya kutoa. Je! lini? Wakati wa siku ya kwanza ya juma. (Jumapili) Je! nani atoe? Kila mmoja wenu anapaswa kutoa. Utoaji ni sehemu ya ibada. Je! kiasi gani? Toa jinsi Mungu alivyokupatia. Iwapo Mungu amekuwezesha kuwa na mali nyingi, basi utatakiwa kutoa zaidi. Iwapo una mali kidogo, utatakiwa tena kutoa kulingana na kidogo ulichonacho.

Soma 1 Wakorintho 6:19-20. Miili yetu ni karama kutoka kwa Mungu. Sisi waamini, miili yetu ni makao ya Roho Mtakatifu. Yote tufanyayo kwa kutumia miili tuliyopewa na Mungu, humtukuza Mungu au Shetani.

Hili ni fundisho muhimu kwa wanafunzi wako. Hupata majaribu mengi ya kutumia vibaya miili yao na akili kwa kutumia madawa ya

kulevywa, pombe, sigara, sinema mbaya, vitabu na lugha mbaya. Unaweza kuwahimiza wampendeze Mungu kwa kutunza miili ambayo wamepewa na Mungu.

Uwakili wa maisha unahusu mambo mengi, sio tu pesa na miili yetu. Tunapaswa kuwa mawakili wema wakati na uwezo wetu. Mungu hutusaidia kuutumia vyema wakati wetu tunaobaki nao tunapomwacha atapangie wakati wetu. Yeye hutubariki pia tunapotumia uwezo wetu kwa kumtukiza.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwawezesha wanafunzi kutambua kwamba wao na vyote walivyonyavyo ni mali ya Mungu ambaye anawataka wawe mawakili wema wa karama zake.

KULIFUNDISHA SOMO

Andika swali hili ubaoni, "Je! wakili ni nani?"

Uliza: Je! siku hizi tunawapata mawakili wapi? (Hotelini, katika mikahawa, katika ndege au melini.)

Uliza: Je! mawakili hufanya nini? (Huhudumia na kutunza mali za watu wengine.)

Andika maelezo yafuatayo chini ya swali uliloandika ubaoni: Wakili ni mtu ambaye anasimamia mali ya mtu mwingine.

Sema: Yusufu wa Agano la Kale ni mfano mzuri wa wakili. Yusufu alianza kufanya kazi katika nyumba ya Potifa, mkuu wa askari wa mfalme. Potifa alimwamini Yusufu sana, na

akamfanya awe msimamizi wa vyote alivyokuwa navyo. Vitu hivi havikuwa mali ya Yusufu, lakini alikuwa wakili wa mali ya Potifa na kusimamia mali yake.

Sema: Paulo katika Agano Jipya, amezungumzia kuhusu yeye mwenyewe kama wakili. Hebu sikiliza ili ujue alikuwa wakili wa nini kwa Mungu.

Fungua Biblia yako katika 1 Wakorintho 4:1-2 na umwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi.

Uliza: Je! Paulo alikuwa wakili wa nini? (Wakili wa siri za Mungu.)

Sema: Paulo alikuwa amewapa ukweli wa Kiroho ambao Mungu alikuwa amempa wajibu wa kuushiriki na wengine.

Twajifunza katika somo letu la leo kwamba sisi ni mawakili wa Mungu. Aliumba kila kitu na ulimwengu wote, na sisi pamoja na vyote tulivyonyavyo ni mali yake.

Andika maneno yafuatayo ubaoni:

Mwenyewe mmoja - Mungu

Mawakili wengi - Sisi

Uliza: Je! Sisi ni mawakili wa nini kwa Mungu?

Ikiwezekana chora picha ifuatayo au tafuta picha za kuonyesha pesa, saa, mtu, na gitaa, au chombo kingine cho chote cha muziki.

SISI NI MAWAKILI WA:

PESA ZETU (mali zetu)

WAKATI

MIILI (na nafsi)

UWEZO (vipawa)

Uliza: Je! tutakuaje mawakili wema wa pesa zetu? (Wape muda wa kujibu, halafu waonyeshe jinsi ya kutoa zaka (fungu la kumi) kwa kutumia sarafu za mapeni kumi. Halafu waambie wanafunzi wawili wasome Maandiko haya: Malaki 3:10a na 1 Korintho 16:2. Mungu ni Mkarimu. Kila kitu ni mali yake na anatutaka tumrudishie tu sehemu moja ya kumi.

Andika maneno yafuatayo ubaoni na uwape wanafunzi muda wa kutosha kuweza kujibu maswali ya Maandiko haya mawili yahasuyo kutoa zaka.

Je! Tutatolea wapi? Lini? Nani atoe? Atoe kiasi gani?

Uliza: Tutaifanyaje iwapo hatuna pesa? Je, tunatakiwa tu tutoe zaka?

Sema: Tunaweza kutoa zaka kwa kumpa Mungu sehemu ya kile tulichonacho. Iwapo tuna shamba, tunaweza kuuza kila mazao ya mstari ya kumi na tutoe pesa hizo kanisani. Nao vijana wanaweza kutafuta kazi ya kibarua na hatimaye watoe zaka ya zile pesa wapatazo.

Uliza: Je! sisi tuaje mawakili wa wakati wetu? Sisi sote hatuna pesa kiasi kimoja, lakini sote tuna wakati sawa.

Uliza: Je! ni mambo yapi mema ambayo wakili mwema atayafanya

katika wakati alionao? (Tumia mfano wa Lilly na Elizabeth ulioko katika kitabu cha mwanafunzi.)

Uliza: Je! umetambua pia kwamba wewe ni wakili wa mwili wako? Mungu alikuumba nawe ni mali yake. Naye yuaishi ndani yako katika umbo la Roho Mtakatifu kwa sababu u Mkristo. (Mwambie mmoja wao asome 1 Wakorintho 6:19-20)

Uliza: Je! mwili wako ni msafi, mtakatifu, na makao mazuri ya Mungu?

Sema: Semeni baadhi ya yale tuwezayo kufanya ili tuifanye miili yetu kuwa mizuri, na mahali pema pa Mungu kuishi. (Tuifanye miili yetu kuwa safi, kufanya mazoezi, kula chakula bora, kutokunywa pombe, kutovuta sigara au kutumia madawa ya kulevya, kusoma vitabu vizuri, kufikiria mambo mema na kadhalika.)

Hebu ufikirie mwili wako ninapokuuliza maswali haya:

1. Akili yangu ni mali ya Mungu. Je! ninayafikiria yaliyomema?
2. Macho yangu ni mali ya Mungu. Je! huwa nampendeza Mungu kwa yale nisomayo na kuona.
3. Mikono yangu ni mali ya Mungu. Je! Mungu huwa anatukuzwa siku zote na jinsi ninavyotumia mikono yangu.
4. Miguu yangu ni mali ya Mungu. Je! huwa naenda mahali pale ambapo Mungu hufurahia kuwa?

Uliza: Je! sisi tukoje mawakili wa vipawa au uwezo wetu?

Sema: Mungu amempa kila mtu uwezo wa kufanya kitu fulani bila shida. Tunaweza kutaka kutumia uwezo huu kwa kumpendeza shetani, au kwa kumtukuza kiroho. (Tumia mfano wa mtu awezaye kuimba vizuri jinsi awezavyo kutumia kipawa chake kwa ajili ya Shetani au Kristo-Bwana.)

Uliza: Je! utaamua leo kumrudishia Mungu akili hii ili aiendeleze na itumie kwa kumtukuza?

KAZI YA KUFANYA

Andika herufi ya K (kosa) kando ya sentensi ambayo si ya kweli, na herufi ya S (sawa) kando ya sentensi ambayo ni ya kweli.

K Watu wazima tu ndio wanapaswa kuwa mawakili.

K Ni lazima mtu awe tajiri ndipo awe wakili mwema.

S Sisi ni mawakili wa miili yetu.

K Mawakili hutunza tu pesa walizonazo.

K Maskini hawezi kuwa wakili.

Andika vizuri herufi zifuatazo ili ugundue yale ambayo sisi ni mawakili wake.

TIWAKA

WAKATI

PAES

PESA

KAILI

AKILI

ILIMI

MIILI

Chora mviringo kwenye maneno ambayo yatakamilisha vyema sentensi hii.

mtu ambaye anamwibia mwajiri wake.

Wakili ni mtu ambaye anafanya kazi ya usafi wa nyumbani ili alipwe.

mtu ambaye anasimamia mali ya mtu mwingine.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Bali tafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa” (Mathayo 6:33).

Uliza: Je! ni nini cha muhimu zaidi maishani mwako? Je! ni mtu, kitu

ulichonacho, tamaa ya kwenda shuleni, umbo lako au kitu kingine? (wape wanafunzi hao muda wa kujibu, au kuandika vitu ambavyo vimechukua nafasi ya kwanza maishani mwao.)

Waambie waseme amri iliyoko katika kifungu cha kukumbuka.

Waambie waseme ahadi iliyoko katika kifungu cha kukumbuka.

Uliza: Je! kumfanya Mungu na ufalme wake uwe wa kwanza maishani kunawezaje kutusaidia kuwa mawakili wema?

WAKATI WA MWISHO

Funga na maombi.

SURA YA KUMI NA MBILI

MWABUDU MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 4:16-22

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wanajua umuhimu wa kumwabudu Mungu kanisani? Vijana wengi hawajui tofauti iliyoko kati ya kukutana na Wakristo wengine kwa ajili ya ushirika na kuabudu kanisani.

Haikosi wanafunzi wako wamewahi kuwasikia watu wazima wakisema kwamba, "Naweza kumwabudia Mungu mahali po pote. Kwa nini niende kanisani?"

Somo hili limetayarishwa ili kuonyesha umuhimu wa kumwabudu Mungu pamoja na waamini wengine tukiwa kanisani. Ulikuwa mpango wa Mungu naye Yesu alifanya hivyo alivyokuwa hapa duniani.

Omba ili upate hekima ya kuweza kufundisha somo hili. Wanafunzi wako wanapaswa kujua mafundisho yahasuyo ibada katika kanisa.

Tayarisha vijikaratasi vidogo vidogo vilivyoandikwa kwa Maandiko haya. Utapaswa kuwaambia wanafunzi wavisome wakati wa somo hili. Zaburi 27:4; Zaburi 55:14; Zaburi 77:13; Zaburi 122:1; Zaburi 149:1; Habakuki 2:20.

Soma Luka 4:16-22. Maandiko haya yanahusu hasa nyumbani kwa Yesu, yaani Nazareti, huko Galilaya. Palikuwa ni mahali ambapo alikuwa

amejulikana sana na wana kijiji. Kwa hivyo, kuwepo kwake katika sinagogi wakati wa sabato hakukuwa jambo la ajabu. Alionekana hapo mara nyingi alipohudhuria ibada.

Yesu alikuwa akihubiri, na kufundisha, na kuwaponya watu katika sehemu nyingine za Galilaya. Alikutana na Simoni Petro, Andrea, Yakobo na Yohana alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya huko Kapernaumu. (Marko 1:16-20) Lakini hii ilikuwa mara yake ya kwanza kwenda nyumbani kwao tangu alipoanza huduma yake.

Haikosi kuwa Yesu alikuwa na maono mengi alipokuwa anarudi kwao. Watu walikuwa wakimfahamu kuwa ni seremala pala mjini kwao, na sasa wangemtambua kwa njia nyingine. Je! wale watu walio-mfundisha akiwa mtoto wangem-sikiliza kwa sasa?

Desturi yake ilikuwa ni kuabudu wakati wa sabato. Jambo hili ni muhimu sana. Bila shaka angeweza kuhudhuria sinagogi kama wale vijana wengine wa Kiyahudi. Walipoenda katika sinagogi walishauriwa kulingana na Maandiko. Palikuwa pia mahali walipojifunzia kusoma na kuandika, na kuelewa desturi zao walizozitii. Wazazi wa Yesu walimpeleka katika sinagogi wakati wa sabato ili kuabudu. Hivi ndivyo jamaa zote za Kiebrania zilivyofanya.

Sinagogi ilikuwa tofauti na hekalu. Kulikuwepo na hekalu moja tu pale Yerusalemu. Hekalu lilikuwa mahali ambapo walifanyia ibada pamoja na kutoa dhabihu. Lakini pia kulikuwepo na sinagogi katika kila jamii, na huko walitilia mkazo hasa mafundisho na mashauri ya kidini.

Kila sinagogi ilikuwa na mtawala au kiongozi ambaye alichaguliwa na washiriki. Yeye mwenyewe hakuongoza ibada, bali aliwachagua wale ambao waliongoza ibada. Kila mwanamume aliye mzima alichaguliwa kuongoza.

Kwa kuanza ibada hii, washiriki waliambiwa wasimame na kuangalia Yerusalemu ili waombe. Hii ilifuatiwa na usomaji wa maandiko kutoka katika sheria yaani kitabu kimojawapo kati ya vile vya kwanza vitano vya Agano la Kale. Yule aliyesoma angetoa maelezo mafupi juu ya yale aliyosoma. Baada ya hapo walisoma kutoka katika vitabu vya manabii. Walimalizia ibada kwa maombi na kuwabariki watu. Palikuwepo na mahali ambapo palitengenezwa kwa ajili ya kutolea sadaka ya kuwapatia maskini wakati walipokuwa wakitoka nje.

Yesu alisoma katika maandiko ya nabii Isaya. Hakupewa kitabu bali alipewa hati ya kuviringisha. Pengine Yesu alitaka apewe maandiko ya Isaya kwa sababu msomaji ndiye aliyechagua mahali ambapo angesoma kutoka kwa manabii.

Yesu alifungua katika Isaya 61 na akasimama ili asome. Hatimaye alikunja hati ile na akamrudishia mtumishi na akakaa chini. Washiriki walijua kwamba anataka aeleze juu ya maandiko yale wakati walipomwona akikaa chini. Je! unaweza kufikiria jinsi washiriki wale walikuwa na tamaa ya kumsikiliza mmoja kati ya vijana wao akiongea? Kila mmoja alimwangalia Yesu.

Yesu alitumia Maandiko yale kujielezea mwenyewe. Alisema kwamba yule Masihi ambaye walikuwa wakimtarajia kwa muda mrefu alikuwa amekuja. Hapo mwanzoni washiriki wale walimsifu sana Yesu, lakini baadaye walianza kufikiria juu ya yale aliyokuwa amesema, na wakapandwa na hasira.

Je! Yesu alifanya nini ambacho kiliwachukiza washiriki wale? Pengine walifikiri kwamba Yesu alikuwa akisema uongo alipotumia Maandiko yale kujielezea mwenyewe. Pia, wakati Yesu alipoeleza yale aliyosoma alitoa mifano alilinganisha na Watu wawili wa Mataifa: mjane aliyeishi kule Serepta ambaye alimsaidia Eliya, na Naamani mtu wa Shamu ambaye aliponywa na Elisha. Wao hawakuwa tayari kuamini kwamba Mtu wa Mataifa alikuwa na sehemu katika Ufalme wa Mungu.

Ingekuwa tofauti iwapo mgeni angesema hivyo, lakini si yule ambaye ni mmoja kati ya vijana wao. "Je!

huyu siye mwana wa Yusufu?" Wakauliza. Atakuwaje ndiye Masihi? Yesu aliendelea kuwaambia, "Amini, nawaambie ya kwamba, hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe..."

Pengine huu ndio uliokuwa wakati wa huzuni sana kwa Yesu. Alikataliwa na akataka kuuawa na wale waliomfahamu sana. Yesu alitoweka na akaenda zake hadi Kapernaumu.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwahimiza wanafunzi kuwa na desturi ya kwenda kanisani kila Jumapili ili kuabudu.

KULIFUNDISHA SOMO

Utatayarisha wanafunzi kwa kuwagawa katika makundi mawili. Liambie kila kundi litayarishe ibada ya kanisa. Wape muda kidogo wa kujitayarisha halafu umwambie mmoja kutoka katika kila kundi asomee darasa kile walichojadiliana.

Andika ubaoni wakati kila kundi litoapo orodha ya yale yaliyoko katika ibada hiyo. Mfano wa yale yanayohitajika ni: maombi, sifa, kuimba nyimbo, kusoma Neno la Mungu na kuhubiri.

Uliza: Je! ibada ni nini? (Wape muda wa kujibu. Ni hali ya kumfahamu Mungu.)

Uliza: Je! tunapaswa kuabudu wapi? (kanisani)

Sema: Tunaweza kumwabudia Mungu mahali po pote, lakini nyumba ya Mungu, ambayo ni kanisa, ndipo mahali panapofaa sana kufanyia ibada.

Uliza: Je! kwa nini mnafikiri ni muhimu kumwabudu Mungu katika jengo la kanisa? (Tangu Mungu alipowaita watu wake kule Misri aliwapangia mahali ambapo wangepanyia ibada.)

Eleza kwa ufupi jinsi Mungu alivyopangia kujengwa kwa maskani matakatifu (Kutoka 25:9) na baadaye jinsi ya kujenga hekalu la Yerusalemu (1 Wafalme 6). Kuna maelezo katika kitabu cha wanafunzi.)

Wape wanafunzi vile vijikaratasi ambavyo uliandika Maandiko uliyopewa ili wayasome.

Uliza: Je! Yesu aliabudia wapi alipokuwa hapa duniani? (Katika hekalu kule Yerusalemu na katika sinagogi kule alipoishi na kufundisha.)

Mwambie mwanafunzi asome Luka 4:16-22.

Sema: Mnapaswa kufahamu kwamba Yesu alikuwa akihudhuria ibada za sinagogi kila wakati wa sabato. Alikuwa amezoea hivyo tangu alipokuwa mdogo, na aliendelea tu hivyo hata baada ya kuwa mtu mzima.

Uliza: Je! Yesu angekuwa kama mgeni katika sinagogi alipokuwa kijijini (mjini) kwao? (La, angekuwa anajulikana sana.)

Uliza: Je! unafikiri ni kwa nini Yesu alichaguliwa kusoma Maandiko wakati ule wa sababo? (Sababu moja ni kwamba Yesu alikuwa amejulikana sana kwa sababu ya mafundisho yake, mahubiri na jinsi alivyowaponya watu kule Galilaya.)

Fanyeni mchezo wa kuigiza wa hadithi hii. Mwambie mwanafunzi mmoja awe "Yesu". Mwambie kwamba atakuwa kati ya wale watakaoingia katika sinagogi. Atachukua hati ya kuviringisha kutoka kwa mtumishi, atafute mahali fulani, akiisha pata asimame na asome. Halafu akae chini na aanze kueleza yale aliyosoma.

Mwambie mwanafunzi mwengine awe "mtumishi" ambaye anaitunza ile hati ya kuviringisha.

Mchague mwanafunzi mwengine awe "kiongozi wa sinagogi". Amwambie Yesu asome kutoka katika Manabii na awaelezee washiriki maana ya maandiko yale.

Wachague wanafunzi wengine wawe mama wa Yesu, ndugu zake na dada ambao wamehudhuria ibada hiyo.

Wanafunzi wote waliobakia wawe washiriki. Watatakiwa wafurahi baada ya Yesu kuwaelezea, halafu waanze kuzungumzana kati yao. Mwishowe watasimama na wajifanye kuwa wamekasirika sana wanapomtoa Yesu nje ya sinagogi.

Mchezo huu utaisha huku Yesu akisema kwamba, "Hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe."

Sema: Mfano huu wa Yesu unapaswa kuwakumbusha kuzoea kuabudu katika nyumba ya Mungu mara kwa mara. Jambo hili lilikuwa muhimu kwa Yesu, nalo lapaswa liwe la muhimu kwenu pia.

KAZI YA KUFANYA

Weka alama (✓) kwenye jibu lililo la kweli.

Yesu alienda mara kwa mara kuabudu

✓ katika sinagogi.

—shambani.

—katika soko la Nazareti.

Jaza nafasi zilizoachwa. Maandiko yenyewe ni ya Luka 4:16a.

"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome."

Chora mviringo juu ya njia ambazo ninyi hutumia kwa kuabudu katika kanisa lako.

kuzungumza na rafiki.

kusikiliza mahubiri

kusoma Biblia

kuomba

kuimba nyimbo

kuandika

kutoa sadaka

kula peremende

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Wala sisi hatutaiacha nyumba ya Mungu wetu" (Nehemia 10:39b).

Uliza: Je! mnafikiri neno "kuiacha" nyumba ya Mungu linamaanisha nini? (Kutoenda kuabudu kanisani, kutofanya usafi kanisani.)

Andika baadhi ya sababu ambazo zitakufanya kutoacha nyumba ya Mungu, katika nafasi ifuatayo.

(Jibu la mwanafunzi)

WAKATI WA MWISHO

Sehemu nyingine ya ibada tufanyayo kanisani hudhihirishwa na vitendo vyetu. Huwa hatumpendezi Mungu iwapo tutazungumza na

marafiki, au tukiandikaandika katika vitabu vya kanisa na kwenye viti, au kutosikiliza wakati wa ibada.

Hii ni nyumba ya Mungu, nasi tunapaswa kuwa na heshima tuwapo humo. Ugawe darasa lako katika makundi mawili kama iwapo nafasi. Liambie kundi moja lionyeshe njia nzuri ya kutenda kanisani. Liambie lile lingine kuonyesha matendo mabaya.)

Funga kwa maombi.

SURA YA KUMI NA TATU

KUHESHIMU NYUMBA YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Zaburi 122:1; 46:10; 51:1-2; 100

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wao huwa na heshima wawapo kanisani? Au, wao hufanya kelele wakiingia na kutoka nje wakati wa ibada? Je! wao hutunza mali (vifaa) ya kanisa na husaidia kuvifanya viwe visafi? Au, wao huwaambia wenzao wajibu huo?

Lifikirie kanisa lako. Je! hutoa sifa nzuri kwa wale ambao si washiriki wake? Je! Nyasi huwa zinakatwa? Je! maua yanakuzwa kando ya kanisa hilo? Jengo la kanisa ni muhimu sana. Ni nyumba ya Mungu. Nasi tunapaswa kuitunza.

Ombea matayarisho yako ya somo hili. Mwombe Mungu akusaidie ili uwatie moyo wanafunzi kuweza kufanya ibada ambayo inampendeza Mungu.

Soma Maandiko na uyaache yazungumzane na moyo wako kabla ya kuwafundisha wanafunzi ukweli huu. Habari hii yote imetoka katika Zaburi, kitabu cha nyimbo za Waebrania. Zaburi hii iliandikwa kama shairi naye huzungumzia kila hali ambayo sisi hupitia. Zaburi hii ingali ya muhimu kwetu leo hata ingawa iliandikwa zamani sana.

Hebu zifikiri nyimbo zilizotolewa kwa Maandiko ambazo unazijua, na uwe tayari kuziimba pamoja na

wanafunzi wako. Nyimbo zifuatazo ni nzuri sana kwa kutumiwa katika somo hili, "This is the Day", "Rejoice in the Lord Always", "I was Glad When They said Unto Me."

Soma Zaburi 122:1.

Zaburi hii inahusu kanisa la Yerusalemu. Twajifunza ukweli fulani uhusuo ibada kutoka kwa vifungu.

1. Mwandishi wa zaburi aliingia katika nyumba ya Mungu akiwa mwenye furaha.
2. Watu walienda kuabudu katika nyumba ya Mungu. Watu wengi husema kwamba wanaweza kumwabudu Mungu wakiwa nyumbani kwao na pia katika kanisa. Ni kweli kwamba tunaweza kumwabudia Mungu mahali po pote, lakini ni vyema zaidi tunapomwabudia Mungu ndani ya nyumba yake.
3. Watu hao waliabudu pamoja. Idadi ya watu inaweza kuwa chache au nyingi, lakini wanapokutanika huwa wanatiana moyo na kuhimizana.

Soma Zaburi 46:10. Ni vigumu kwetu kutulia na kumsikiliza Mungu ili anene nasi. Huwa kila mara tunaenda huku na huko, tunaongea, tunafanya kazi zetu au tunasikiliza muziki. Sisi huishi katikati ya makelele, lakini tunapaswa kumpangia Mungu wakati wake.

Mwandishi wa zaburi alizungumzia yale aliyoyapitia yeye mwenyewe na akatoa hitaji letu la siku hizi. Jinsi tunavyopaswa kuacha, na kumtazama Mungu, na kumsikiliza. Tutamfahamu vizuri iwapo tutakuwa mbele zake kila wakati.

Soma Zaburi 51:1-2. Kutubu ni sehemu ya ibada. Dhambi zetu ni pingamizi kwa sababu zinazuia ushirika wetu na Mungu hata hawezi kutusikia. Sisi hujiona jinsi tulivyo wenye dhambi na kuwa hatufai tunapouangalia utakatifu wa Mungu.

Zaburi ya 51 iliandikwa na Mfalme Daudi na inaonyesha jinsi alivyotubu dhambi zake. Alisema kwamba, "Ee Mungu unirehemu, unitakase dhambi zangu!"

Ni lazima tumwombe Mungu msamaha wa dhambi zetu iwapo tunataka tufanye ibada ambayo itampendeza. Halafu tutapokea huruma zake kwa imani yetu, na kumshukuru kwa kututakasa.

Soma Zaburi 100. Maandiko haya ni baadhi ya yale yanayofahamika sana katika zaburi. Unapaswa kuyajua kwa moyo iwapo bado hujajifunza. Zaburi hii ni amri pamoja na ushuhuda.

Mwandishi wa zaburi anaanza kwa kuiambia dunia yote imfanyie Bwana shangwe ya furaha. Mwito wa yule anayeabudu ni kufanya ibada, kuimba na kutoa shukrani. Anaendelea kwa kusema kwamba Bwana ndiye Mungu, nasi tu watu wake. Yeye ni mwema, hebu tumsujudie na kumshukuru.

Ni lazima Wakristo wajaribu wawezavyo kulifanya kanisa kuwa mahali pa kuabudia sisi huonyesha shukrani na furaha yetu. Ibada si jambo la huzuni. Ibada i hai na ya furaha kwa sababu tunamtumikia Mwokozi aliye hai na ambaye aliyeshinda yote.

Unapoingia katika nyumba ya Bwana kila Jumapili, unapaswa kufanya hivyo kwa roho ya furaha na shukrani. Hali yako itawasaidia wenzako kupata furaha hiyo hiyo.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kuwa na heshima katika nyumba ya Mungu na kujionea ibada ya kweli.

KULIFUNDISHA SOMO

Anza somo la leo kwa kuimba nyimbo kutoka kwa Maandiko. Mhimize mwanafunzi mmoja aongoze, lakini pia unapaswa kuwa tayari kuongoza ikiwa hatatokea ye yote ambaye yuko tayari.

Sema: Somo letu la leo lapatikana katika Zaburi, kitabu ambacho kilikuwa cha nyimbo za Waebrania.

Uliza: Je! mnaweza kufikiria jinsi ilivyokuwa kwamba Biblia zetu zilitumiwa kama kitabu cha nyimbo na pia kwa kusoma Maandiko?

Sema: Zaburi ilitumiwa wakati wa ibada, na hii ndiyo tunayotaka tujifunze tena leo.

Mwite mwanafunzi mmoja aje mbele na umwambie aandike baadhi sehemu za ibada walizojifunza wiki iliyopita. (Ibada ni pamoja kutoa sifa, kuimba

nyimbo, kuomba, kusoma Neno la Mungu, kusikiliza mahubiri ya neno la Mungu, na kutoa sadaka.)

Uliza: Je! katika somo letu la wiki iliyopita tuligundua kwamba ibada ina maana gani? (Kupata ufahamu wa Mungu)

Sema: Maandiko yetu ya kwanza ni Zaburi 122:1. (Mwambie mwanafunzi mmoja ayasome).

Uliza: Je! ni hali ipi ambayo mwandishi wa zaburi anaizungumzia katika kifungu hiki? (Furaha)

Uliza: Je! ni nini kinachomletea mwandishi furaha? (Kwa sababu alikuwa akienda katika nyumba ya Mungu.)

Sema: Zaburi hii ilikuwa ikiimbwa wakati watu walipokuwa wakiingia katika hekalu la Yerusalemu. Ni vizuri kufahamu tuni ambayo Waebrania walitumia, lakini pia tunaweza kuwa na yetu. (Imbeni pamoja kifungu hiki mkitumia tuni ambayo wote mnaifahamu.)

Fanyeni mchezo aina mbili wa kutoka kwa kifungu hiki: Mwambie mwanafunzi mmoja aje darasani (kanisani) akiwa anaimba kwa furaha. Hali mwingine aje ndani akiwa ameinamisha kichwa chake na ajifanye kuwa amebeba mzigo mzito. Waambie wanafunzi hao kwamba wenzetu wanaweza kuvutwa. Furaha huambukizana.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome Zaburi 46:10.

Uliza: Je! kifungu hiki kinatuambia tufanyaje baada ya kuingia kanisani

tukiwa wenye furaha? (Tuwe watulivu.)

Sema: Hili ni fundisho ambalo linapaswa kufahamika vizuri. Tunapaswa kufahamu kwamba tunatakiwa kuwa na heshima tufikako katika nyumba ya Mungu. Huwa tunaenda humo kumwabudu na kusikiliza neno lake. Ni vizuri kuwa na ushirika na washiriki wengine. Lakini, tutakuwa na muda mwingi wa kuzungumza nao baada ya ibada. Kufanya ibada ni wakati wa kuzungumza na Mungu na kumsikiliza akinena nasi kupitia kwa Neno lake.

Mungu hupata shida kutufanya tumsikilize ili atwambie kile ambacho tunapaswa kusikia. Huwa tuna kazi nyingi ya kutoweka kungojea na tumsikilize.

Utapaswa leo uingie kanisani kwa roho ya utulivu. Unapaswa kuona kuwepo kwa Mungu umtarajie kusema nawe kupitia kwa wale wanaoongoza ibada hiyo.

Kifungu hiki hakizungumzii tu kanisa, bali hata kwa ibada za kibinafsi ambazo huwa tunafanya manyumbani mwetu. Anatumia tuwe watulivu ili tuweze kumfahamu vizuri.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome Zaburi 51:1-2.

Sema: Vifungu hivi tunavyojifunza vya Zaburi vyote vinaelekeana. Kwanza tulijifunza kwamba tunapaswa kuingia katika nyumba ya Mungu tukiwa wenye furaha halafu tungejee katika hali ya kutulia.

Uliza: Je! kulingana na kifungu hiki ni hatua ipi inayofuata wakati wa ibada? (kukiri au kutubu)

Sema: Biblia inasema kwamba dhambi hututenganisha na Mungu naye hawezi kutusikia. Ni lazima tutubu dhambi zetu ili tufurahie ibada na kwenda mbele za Mungu tukiwa na mioyo iliyotakaswa. Daudi ndiye mwandishi wa Zaburi hii, naye alimwomba Bwana amrehemu na amtakase.

Mwambie mwanafunzi mwengine asome Zaburi 100.

Uliza: Je! unaweza kutambua amri zilizoko katika vifungu hivi? Hebu iseme. (Mfanyieni Bwana shangwe, mtumikieni Bwana, njoni mbele zake, mjueni Bwana, na kadhalika.)

Uliza: Je! mwandishi wa Zaburi anatoa ushuhuda upi unaomhusu Bwana? (alituumba, tu watu wake, yeye ni mwema, rehema na uaminifu wake ni wa milele)

Sema: Zaburi hii ni wimbo wa sifa na kutoa shukrani. Hii pia ni sehemu muhimu katika ibada yetu. Huwa tunamsifu tunapoimba, tunapoomba, kupitia kwa hali yetu ya ibada na kwa maneno tusemayo. Mungu ni mwema nasi tunamsifu kwa sababu anastahili sifa.

KAZI YA KUFANYA

Kata kwa mstari maneno yaliyo na kosa katika sentensi zifuatazo.

1. Tunapoingia katika nyumba ya Mungu tunapaswa (~~kuzungumza na rafiki zetu~~, kuzungumza na Mungu.)

2. Ni lazima (tumsikilize mhubiri, ~~tuwasikilize rafiki zetu~~) tuwapo katika nyumba ya Mungu.

3. Tunapaswa kutoa (zaka na sadaka, ~~mbwa na viatu vichafu~~) tuwapo kanisani.

4. Mchungaji hutupa (~~mafundisho yake~~, ujumbe wa Mungu.)

5. Tunapaswa (kutunza, ~~kuharibu~~) vitu na jengo la kanisa.

Weka alama (✓) kwenye jibu lililo sawa. Je! Mungu anatumia tufanyaje tuendapo katika nyumba yake?

_____ tulale _____ tuzungumze na rafiki zetu ✓ tumsifu kwa nyimbo

Hapo chini kuna zaburi 100. Chora mviringo kwenye maneno yafuatayo: mfanyieni Bwana shangwe, mtumikieni, njoni, jueni, ingieni, mshukuruni, lihimidini. Mnapaswa kufahamu kwamba maneno haya ni amri, au vitendo ambavyo tunapaswa kufanya mioyoni mwetu.

(Mfanyieni Bwana shangwe) dunia yote;

(Mtumikieni) Bwana kwa furaha;
(Njoni) mbele zake kwa kuimba;

(Jueni) kwamba Bwana ndiye Mungu;

Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake;

Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake.

(Ingieni) malangoni mwake kwa kushukuru;

Nyunani mwake kwa kusifu;

(Mshukuruni, lihimidini) jina lake;

Kwa kuwa Bwana ndiye mwema;
Rehema zake ni za milele,
Na uaminifu wake vizazi na vizazi.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu" (Zaburi 46:10).

Sema: Sisi humfahamu Mungu kwa kuwa nawe mara kwa mara. Je! umepanga wakati ambao wewe hukutana na Mungu kila siku?

WAKATI WA MWISHO

Yafikirie mambo haya tuliyojifunza leo wakati unapoenda kuabudu katika nyumba ya Bwana:

1. Mnapaswa kwenda humo mkiwa na furaha mioyo mwenu.
2. Unapaswa kutulia na kumwacha Mungu aseme nawe.
3. Tubu dhambi yo yote ambayo inatutenganisha na Mungu.
4. Mwabudu Mungu kwa kumsifu kwa nyimbo na maneno ya shukrani.
5. Uwe tayari kumtumikia.